




Padre aeleza Ijumaa Kuu, maana yake na inavyosherehekewa

UKURASA 19



LEO RAMADHANI 13


# Nipashe

Ijumaa Aprili 15, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580916

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# UPIGAJI BOT

**CAG** afichua watumishi wanaokata noti kulipwa bil. 3.9/- wakidai chakavu, ACT Wazalendo yataka waliotajwa wawajibishwe ... *Endelea Uk. 2*









Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, akionyesha mali mbalimbali, ikiwemo shehena ya dawa za kulevya aina ya bangi, zilizokamatwa, wakati wa operesheni maalum ya siku 19, iliyofanywa kwa ushirikiano na mkoa wa Pwani, ambapo watuhumiwa 632 wametiwa mbaroni. **PICHA ZOTE: JUMANNE JUMA**

## 632 mbaroni kwa madai ya uhalifu mikoa ya Dar, Pwani

UKURASA 3

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### WAFUASI WA MFALME ZUMARIDI WAENDELEA 'KUMSALITI', WABAKI 5

MSHTAKIWA Diana Bundala maarufu kama mfalme Zumaridi Mungu chini ya jua, anayekabiliwa na kesi ya kusafirisha binadamu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Mwanza, amebaki wa wafuasi watano mahabusu kati ya 91 walioapa kukaa naye na kukataa dhamana siku ya kwanza walipofikishwa mahakamani.

UKURASA WA 4

### HASARA YA MABILIONI YABAINIKA TANESCO

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini upotevu wa Sh. bilioni 105.49 kutokana na kutoza bei za chini za umeme katika Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

## Neema yaja TAMISEMI bajeti serikali 2022/23

UKURASA 3

**MICHEZO** **MAUNDA ZORRO KUZIKWA KESHO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Katibu wa Baraza la Ulamaa, Sheikh Hassan Chizenga, akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana, kuhusu ufunguzi mdogo wa Msikiti wa Muhammad wa sita Kinondoni, utakaofanyika leo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Upigaji bil. 3.9/- BoT mfumo noti chakavu

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amefanya ukaguzi maalum kuhusu tuhuma za ubadhirifu za noti chakavu zilizorejeshwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na kubaini udanganyifu uliosababisha hasara ya mabilioni ya shilingi.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Jumanne wiki hii, CAG Charles Kichere anasema amebaini tatizo hilo alipokuwa anafuatilia tuhuma za ubadhirifu wa noti chakavu uliofanyika BoT kuanzia Januari 2017 hadi Desemba 2019.

Anasema ofisi yake ilifanya ukaguzi maalum BoT baada ya kuombwa na Naibu Gavana (Utawala na Udhibiti wa Ndani) kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi.

"Lengo la ukaguzi wangu lilikuwa kujua kiasi cha hasara ambacho Benki Kuu ilipata na watu waliohusika katika ubadhirifu huo.

"Kupitia uchunguzi wangu, nilibaini Benki Kuu ilipata hasara ya Sh. bilioni 3.99 kwenye urejeshaji wa noti chakavu.

"Kulingana na sera na miongozo ya Benki Kuu, noti chakavu ni noti halisi yenye kukosa sifa za kufanya malipo halali. Benki Kuu ina mamlaka ya kupokea na kurejesha thamani ya noti mbovu (chakavu) na kutoa noti mpya," anasema.

CAG anafafanua kuwa katika ukaguzi huo, alibaini BoT ilipokea noti za Sh. bilioni 4.17 ambazo ni noti 417,006 za Sh. 10,000 kati ya Januari 2019 na Septemba 2019, ambazo zilidaiwa kuwa chakavu ili zibadilishwe na kutolewa noti mpya.

Kama sehemu ya taratibu za ukaguzi, CAG anasema alipitia na kuhesabu noti zote pamoja na kupitia vigezo vilivyopitishwa na BoT katika kuzipa thamani noti hizo chakavu na kutoa noti mpya.

Anasema katika uchunguzi huo, alibaini kuwa noti 1,427 zenye thamani ya Sh. milioni 14.27 zilikuwa safi na zinafaa, hivyo hazikuwa na sifa ya kuwa noti chakavu.

Pia alibaini kuwa noti 16,187 zenye thamani ya Sh. milioni 161.87 zilikidhi vigezo vya kurejeshwa BoT na kutolewa noti mpya , wakati noti 399,392 zilizobaki zenye thamani ya Sh. bilioni 3.99 hazikuwa na vigezo vya kupewa noti mpya na zilipewa noti mpya kwa njia ya udanganyifu uliofanywa na maofisa wawili na watunza fedha wanne wa BoT.

"Hili lilifanikiwa kwa kupanga na kutoa thamani na kuidhinisha utoaji wa noti mpya kwa njia ya udanganyifu na kuisababishia Benki Kuu hasara ya Sh. bilioni 3.99. Katika uchunguzi zaidi, niligundua kuwa wahusika walikata vipande vya noti 399,392 vyenye thamani ya Sh. 10,000 na kuvibandika kwenye karatasi nyeupe kisha kudai noti mpya.

"Ili kutengeneza na kudai noti mpya, niligundua kuwa vipande 399,392 vilikatwa kutoka kwenye noti 199,696 zilizokuwa safi. Baada ya kufanya uchambuzi wa gharama, ilibainika kuwa Benki Kuu ilitumia kiasi cha Euro 0.0381, sawa na Sh. 103.56 kuchapa na kusambaza noti moja ya Sh. 10,000.

"Kutokana na ubadhirifu huo, Benki Kuu ilipata hasara ya Sh. milioni 20.68 ya kuchapisha na kutoa noti 199,696 zilizotumika katika udanganyifu huo.

"Pia nilibaini kuwa Benki Kuu haikutunza daftari la wateja waliokuwa wanabadilisha fedha chakavu. Kwa hali hiyo, sikuweza kuwatambua wateja waliobadilisha fedha chakavu katika kipindi husika," anabainisha.

**NYENDO WATEJA 24**

Pamoja na vikwazo hivyo, CAG anasema alipitia kitabu cha mahudhurio ya wateja kuanzia Januari 2019 hadi Novemba 2019 na kubaini wateja 24 ambao walikuwa na mtindo wa kutembelea Benki Kuu mara kwa mara kwa ajili ya kufanya miamala ya noti chakavu, ambao wamehusishwa kushirikiana na wafanyakazi wa Benki Kuu kutekeleza mpango huo.

"Maoni yangu ni kuwa ubadhirifu huo umesababishwa na wafanyakazi wa Benki Kuu kukosa uadilifu pamoja na kuwapo kwa upungufu wa udhibiti wa ndani; hivyo kumeisababishia hasara Benki Kuu ya Sh. bilioni 3.99.

"Ninapendekeza Gavana wa Benki Kuu achukue hatua stahiki za kinidhamu dhidi ya wafanyakazi wa Benki Kuu waliohusika katika ubadhirifu huu na kuhakikisha kuwa kunakuwapo na usimamizi madhubuti wa miamala yote ya noti chakavu zinazobadilishwa Benki Kuu na kwenye benki zote za biashara," CAG anasema.

# ACT Wazalendo yataka wahusika Ripoti ya CAG wachukuliwe hatua

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimechambua ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), huku kikionyesha maeneo 10 yaliyoonesha udanganyifu na ubadhirifu wa fedha ambao umeisababishia serikali hasara na kutaka waliohusika wawajibishwe.

Akifanya uchambuzi huo jana mkoani Dar es Salaam, Waziri Kivuli na Msemaji wa Sekta ya Fedha na Uchumi wa ACT-Wazalendo, Emmanuel Mvula, alitaja maeneo hayo yakiwamo fedha kutumiwa bila kupita mfuko mkuu wa hazina jambo ambalo alisema limekuwa tatizo sugu.

Mvula alisema mwaka wa fedha 2019/20 serikali ilitumia Sh. trilioni 2.2 bila kupita kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kubainisha kuwa hoja hiyo imekuwa ikijirudia kwa miaka mitatu mfululizo.

"Matumizi ya fedha za serikali bila kupita kwenye Mfuko wa Hazina ni ukiukwaji wa katiba ya nchi yetu Ibara ya 135 kifungu cha kwanza ambayo inaelekeza kuwa ni lazima kila fedha ya serikali itunzwe kwanza kwenye mfuko mkuu kabla ya kutumika," alisema.

Mvula alionyesha kiwango cha matumizi ya fedha yaliyofanyika kwa miaka mitano ambayo hayakupita kwenye mfuko mkuu wa hadhina ya serikali yakiwamo mwaka 2017/18 Sh. bilioni 800, 2018/19 Sh. trilioni 1.7, 2019/20 Sh. trilioni 2.2 na 2020/21 Sh. trilioni 1.2. Kutokana na hali hiyo, alitoa wito kwa serikali kutofumbia macho tatizo hilo.

Eneo la pili ni madai ya watumishi wa umma Sh. bilioni 429, alieleza kuwa katika kipindi cha miaka saba watumishi wa umma hawajapandishiwa mishahara licha ya gharama za maisha kuongezeka, pia stahiki zao za kisheria serikali haijawapatia kama ambavyo imethibitishwa na CAG kuwa malimbikizo ya madai ya watumishi wa Umma yameongezeka.

Alisema hali hiyo inaondoa morali ya watumishi wa umma kutekeleza wajibu wao wa kuhudumia wananchi na utoaji huduma nchini, huku akiishauri serikali kuwa iwalipe watumishi wote malimbikizo ya madai yao kwa mkupuo ili kuwawezesha kukabiliana na gharama za maisha ambazo zimeendelea kupanda.

Eneo la tatu, alisema ni madai ya wazabuni kwa serikali huku akitoa mfano wa kuongezeka akionyesha mwaka 2020/21 yalikuwa Sh. trilioni 3.6 kutoka Sh. trilioni 3.1 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la Sh. bilioni 500.

Eneo la nne ni ubadhirifu wa Sh. bilioni 279.5 katika miradi mbalimbali ya maendeleo. Alisema uchambuzi wao ulibaini ubadhirifu katika miradi mitatu ikiwemo ujenzi wa vihenge Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) katika bandari ya Tanga na mradi wa Mkulazi.

Eneo la tano ni uvunjaji mikataba kiholela, ambao umesababisha nchi kupata hasara ya Sh. bilioni 47, alieleza kuwa katika kipindi cha miaka ya karibuni kumekuwa na mwenendo wa viongozi wa serikali kusitisha kiholela mikataba ambayo taasisi zake ziliingia na makampuni binafsi kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali.

Alisema katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Nishati Vijijini (REA), NFRA na Jeshi la Magereza walikatisha mikataba mitatu yenye thamani ya Sh. bilioni 126.55 kutokana na wakandarasi hao kutofanya kazi vizuri, jambo ambalo limeisababishia serikali hasara.

"Tuinaitaka serikali kuheshimu mikataba na kufuata taratibu za sheria kama inatakiwa kusitisha mikataba husika ili kuepuka hasara kama hizi. Taasisi za serikali ziepuke kufanya maamuzi bila kupata ushauri wa kisheria wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali," alisema Mvula.

Eneo la sita, alisema CAG alifanya ukaguzi maalumu katika Mamlaka ya Bandari Tanzania na kubaini ubadhirifu wa Sh. Bilioni 71, ambao ulihusisha bandari ya Mwanza na Dar es Salaam ambapo fedha za umma zilikuwa zinahamishwa kupelekwa Mwanza na kutumiwa bila kufuata taratibu.

Eneo la saba alisema ni Mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere unaogharimu Sh. trilioni sita aliodai kuwa unatekelezwa kiholela, huku akitoa wito kwa serikali kufanya marejeo ya mradi huo na kupendekeza namna bora zaidi za kuutekeleza ili kuwa na manufaa kwa nchi.

Eneo la nane ni madai na madeni ya mashirika ya umma, alisema CAG pia alionyesha mashaka katika suala la ukusanyaji duni wa madai ya mashirika hayo uliosababisha kuwa na madai kwa mashirika 93 Sh. trilioni 3.71 na kuchelewesha maendeleo ya mashirika hayo katika kuchochea ukuaji wake na ukuaji wa uchumi wa nchi.

## 632 mbaroni tuhuma za uhalifu Dar, Pwani

**Na Romana Mallya**

OPERESHENI maalum iliyofanywa kwa ushirikiano wa Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Mikoa ya Pwani na Rufiji imewatia mbaroni watuhumiwa 632 wakiwa na bunduki tano na risasi 53.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema watuhumiwa hao wamekamatwa kwa tuhuma mbalimbali ikiwamo unyang'anyi wa kutumia silaha.

Alitaja makosa mengine kuwa ni wizi wa magari, pikipiki na bajaji, unyang'anyi wa kutumia nguvu, dawa za kulevya za kiwandani na mashambani, unyanganyi na kuiba na wizi wa mifugo.

Kamanda Muliro alisema operesheni hiyo imefanyika kwa siku 19 kuanzia Machi 21 kwa lengo la kuzuia na kupambana na uhalifu na makosa makubwa.

Alisema watuhumiwa hao pia wamekamatwa na magari tisa, pikipiki 65 za wizi na mitambo ya kutenegeza gongo 15.

"Tumekamata mapipa 70 yenye kimea cha kutengenezea gongo, lita 773 za gongo, dawa za kulevya aina ya heroine kete 88 na gramu 250 na bangi gunia 31, puli 250, kete 5,695, misokoto 1,726.

"Tumezibaini hekari sita za shamba linalolima bangi, kilo 46 za mbegu za bangi na mirungi kilogramu 4.5. Pia tumekamata jino la tembo, vyombo mbalimbali na vifaa vya kieletroniki vilivyotokana na uvunjaji wa nyumba," alisema.

Katika hatua nyingine, Kamanda Muliro alisema wamewakamata watu 1,251 kwa makosa ya usalama barabarani.

"Hairuhusiwi kuendesha gari ukiwa umelewa kwa zaidi ya kiwango cha miligramu 80, hairuhusiwi kuendesha gari la abiria lenye leseni ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ukiwa umelewa, hauruhusiwi kuendesha gari la serikali ukiwa umelewa.

"Katika makosa ya kulipita gari lingine kwenye njia ya hatari tumekamata watuhumiwa 36, mwendokasi 83, kuendesha magari mabovu 840, kutofuata sheria za zebra na taa nyekundu 270, madereva wa serikali tumewakamata 22."

Pia alisema wamewakamata raia 45 wa Ethiopia na Somalia kwa makosa ya uhamiaji, ambao waliwakabidhi Jeshi la Uhamiaji kwa mahojiano zaidi.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, akiwasilisha hotuba ya bajeti ya Ofisi hiyo, kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Neema yaja TAMISEMI bajeti serikali 2022/23

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

NI neema! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka ujao wa fedha.

Katika makadirio hayo yaliyowasilishwa bungeni jijini hapa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Innocent Bashungwa, mradi wa mabasi yaendayo haraka, maarufu mwendokasi, unatarajiwa kutanuliwa zaidi kuyafikia maeneo ya pembezoni mwa Mkoa wa Dar es Salaam ikiwamo Gongo la Mboto.

Vilevile, ofisi hiyo inatarajia kupewa kibali cha kuajiri walimu wapya 10,000; kujenga nyumba za walimu 300; kuongezwa kwa fedha mfuko wa jimbo; na kukarabati jengo la Karikoo lililoungua.

Bashungwa alisema Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza mipango na bajeti ya mwaka 2022/23 kwa kuzingatia vipaumbele 13.

Alivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa elimu msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikijumuisha utekelezaji wa Elimu msingi Bila Malipo, kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi katika mamlaka hizo na kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa huduma za afya ya msingi, lishe na ustawi wa jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Pia kushughulikia malalamiko ya walimu ikiwamo kutopandishwa vyeo kwa wakati na wastaafu kucheleweshewa kulipwa stahili na mafao yao baada ya kustaafu, Bashungwa akifafanua kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu imeanzisha dawati maalum la kupokea malalamiko na kero za wastaafu.

Waziri huyo alisema kipaumbele kingine ni kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi shindani kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji, hasa katika kilimo, mifugo na viwanda.

"Utekelezaji wa jambo hili utahusisha uimarishaji wa sehemu ya uchumi na uzalishaji katika ngazi ya mikoa kwa kuhakikisha kuna rasilimali watu wenye weledi pamoja uwapo wa fedha na vitendea kazi.

"Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa maofisa ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wizara za kisekta ili kuboresha mazingira ya kilimo, mifugo, uwekezaji, viwanda na biashara," alisema.

Bashungwa alisema kipaumbele kingine ni kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi, ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa shughuli za serikali, taasisi, programu na miradi katika ngazi ya mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kusimamia matumizi ya TEHAMA katika ngazi zote za ofisi hiyo.

Vipaumbele vingine ni: kuendeleza rasilimaliwatu katika ngazi zote za Ofisi ya Rais-TAMISEMI; kuratibu ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya maeneo ya utawala ya mikoa, wilaya na halmashauri; kusimamia matumizi ya rasilimali fedha katika ngazi zote; kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D).

**MWENDOKASI KUPANULIWA**

Waziri Bashungwa alisema kuwa kwa mwaka fedha 2022/23, serikali itaanza ujenzi wa awamu ya tatu ya miundombinu ya mabasi yaendayo haraka yenye urefu wa kilomita 24.3 itakayojumuisha barabara za Nyerere hadi Gongo la Mboto, barabara ya Mandela kutoka Tazara hadi makutano ya barabara ya Uhuru na Mandela.

Alisema mradi huo pia utahusisha barabara ya Uhuru kutoka makutano ya barabara ya Mandela hadi makutano ya Mtaa wa Shaurimoyo.

"Mtaa wa Shaurimoyo kutoka makutano ya barabara ya Uhuru hadi Mtaa wa Lindi; Mtaa wa Lindi kutoka makutano ya Mtaa wa Shaurimoyo hadi kituo kikuu cha Gerezani. Kariakoo Nkurumah kutoka makutano ya barabara ya Nyerere hadi makutano ya Mtaa wa Bibi Titi na Mtaa wa Maktaba na Mtaa wa Azikiwe hadi makutano na barabara ya Kivukoni.

"Pa tutakamilisha taratibu za ununuzi mabasi 95 ya nyongeza kwenye awamu ya kwanza ya mwendokasi na kubadilisha mfumo wa uendeshaji na ulipaji wa watoa huduma kutoka kupokea tozo ya kupita katika mfumo wa Dart na kuanza kutumia utaratibu wa malipo ya umbali ambao mabasi yatakuwa yanatembea," alisema.

**AJIRA ZA WALIMU**

Waziri huyo pia alisema kuwa katika kukabiliana na upungufu wa walimu uliopo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeomba kibali cha kuajiri walimu 10,000 wa shule za msingi na sekondari. Kati ya hao, 5,000 ni kwa ajili ya shule za awali na msingi na 5,000 kwa ajili ya shule za sekondari.

Alisema hatua ya kuajiri walimu 10,000 itasaidia kupunguza mahitaji ya walimu wa shule za sekondari kwa asilimia 6.56 na elimu ya awali na msingi kwa asilimia 10.65.

Alibainisha kuwa takwimu zilizopo zinaonyesha kuna jumla ya shule za msingi 17,034 zenye jumla ya wanafunzi 12,033,594 wakiwamo wanafunzi wenye mahitaji maalum 60,825 na shule za sekondari 4,175 zenye jumla ya wanafunzi 2,607,142 wakiwamo wanafunzi wenye mahitaji maalum 11,106.

**BIMA MADIWANI**

Bashungwa pia alisema wanatarajia kujenga nyumba za walimu, kuongeza fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, kutenga fungu kwa ajili ya ofisi za wakuu wa wilaya, kutenga Sh. milini 780 kwa ajili ya kuimarisha usalama mikoa ya mipakani na kutenga Sh. bilioni 10 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Soko la Kariakoo lililoungua huku serikali ikipanga kuchangia Sh. milioni 607.57 kwa ajili madiwani, ikiwamo kuchangia gharama za bima ya afya kwa madiwani.

Ili kutekeleza majukumu hayo, Bashungwa aliliomba Bunge liidhinishe Sh. trilioni 8.779 kwa ajili ya matumizi ya ofisi hiyo na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Alisema Ofisi ya Rais - TAMISEMI, taasisi zilizo chini yake, mikoa 26 na halmashauri 184 inaomba idhini ya kukusanya maduhuli na Sh. trilioni 1.072.

**MATUMIZI UVIKO-19**

Makamu Mwenyekiti Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, Dennis Londo, alisema ufuatiliaji umeonyesha kuwa zipo dalili za baadhi ya halmashauri kutotekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia bajeti badala yake kutumia fedha za UVIKO-19.

Londo alisema ipo pia miradi iliyotekelezwa kwa kutumia fedha zilizotolewa na serikali katika mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi UVIKO-19.

"Ufuatiliaji wa kamati umeonesha kuwa zipo dalili kwamba, baadhi ya halmashauri hazikutekeleza miradi iliyopangwa kwenye bajeti zao, badala yake zimetumia fedha za UVIKO-19 kuendeleza miradi hiyo. Kamati imeona siyo jambo linalofaa," alisema.



Waziri wa Uchukuzi na Ujenzi, Prof. Makame Mbarawa (wapili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) Masanja Kadogosa, wakati wa hafla ya uzinduzi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Tabora hadi Makutupora, Dodoma, iliyofanyika Cheyo B, mkoani Tabora juzi. Wa (pili kushoto) ni Mkuu wa Mahusiano na Mawasiliano wa Benki ya NBC, Godwin Jaha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANESCO yatengeneza hasara ya bilioni 105/- umeme kwa 27,000/-

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini upotevu wa Sh. bilioni 105.49 kutokana na kutoza bei za chini za umeme katika Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Jumanne, CAG Charles Kichere, anasema alibaini shirika lilipoteza Sh. bilioni 105.49 kutokana na kupunguza bei za nishati ya umeme na gharama za uunganishaji wa umeme.

Anabainisha kuwa Sh. bilioni 88.39 hazikukusanywa kutoka kwa wateja 300,697 kwa sababu ya kushusha bei ya kuunganisha umeme mwaka 2020/21 kutoka Sh. 320,960 hadi Sh. 27,000 (kiwango kilichotumika vijijini pekee).

Vilevile, Sh. bilioni 17.1 hazikukusanywa kutoka kwa wateja 208,319 kutokana na kubadilisha madaraja ya matumizi ya umeme kutoka daraja la juu la T1 kwenda la chini la D1 katika mwaka wa fedha 2020/21.

Anasema TANESCO inahitaji tathmini sahihi ya faida na hasara au upembuzi yakinifu kabla ya uamuzi wa kupunguza bei ili kuepusha kukosekana kwa huduma kwa sababu za kukosa fedha za kutosha.

"Ninapendekeza serikali na shirika wahakikishe upembuzi yakinifu unafanyika kabla ya kufanya mabadiliko ya bei na kubadilisha madaraja ya matumizi ya umeme kwa wateja ili kuhakikisha kuna uhimilivu wa shirika katika kutoa huduma," anasema.

**RAKILI ZA MITA ZAIBWA**

CAG pia anasema rakili za mita (Meter Seal) ziligunduliwa katika duka la mtaani kupitia ukaguzi TANESCO, akifafanua kuwa alibaini rakili za mita za umeme 5,000 za shirika kwenye duka hilo na hatua za kisheria zilichukuliwa dhidi ya mwenye duka. "Suala hili linaonyesha kuna udhaifu katika udhibiti na usimamizi wa rakili za mita za umeme katika shirika, hivyo linaweza kupoteza mapato makubwa kutokana na kuibiwa rakili za mita ambazo zinaweza kutumika kuiba umeme.

"Ninapendekeza shirika liimarishe ulinzi na udhibiti wa rakili za mita kwa kuhesabu mara kwa mara idadi yake na kufanya usuluhishi endapo kuna tofauti ya idadi. "Pia ninapendekeza shirika lichunguze mazingira yaliyosababisha rakili za mita kuibwa na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wote waliohusika," CAG anasema.

# Wafuasi wa Zumaridi wazidi 'kumsaliti', wabaki 5

**Na Richard Makore,** MWANZA

MSHTAKIWA Diana Bundala maarufu kama mfalme Zumaridi Mungu chini ya jua, anayekabiliwa na kesi ya kusafirisha binadamu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Mwanza, amebaki wa wafuasi watano mahabusu kati ya 91 walioapa kukaa naye na kukataa dhamana siku ya kwanza walipofikishwa mahakamani.

Wafuasi hao wamezidi kupungua kwa kupata dhamana kila wanapofikishwa mahakamani na kukiuka kauli yao ya awali kwamba wapo tayari kufa naye mahabusu kuliko kukubali kudhaminiwa.

Mpaka jana walikuwa wamebaki washtakiwa watano kati ya 91 waliokataa kudhaminiwa siku ya kwanza Machi 3, mwaka huu, walipofikishwa mahakamani hapo. Wafuasi hao watano ambao dhamana zao mpaka jana zilikuwa wazi wameendelea kushikilia msimamo wao wa kutokubali kudhaminiwa kwa madai kwamba wapo tayari kufa na mfalme wao huko gerezani.

Siku ya kwanza wafuasi 91 walikataa kudhaminiwa, lakini kadri walivyokuwa wakipelekwa mahakamani idadi hiyo ilizidi kupungua na jana walibaki watano ambao bado wameshikilia msimamo wao. Machi 31, mwaka huu, wafuasi hao walikuwa wamebaki saba, lakini jana wawili waligeuka na kukubali dhamana.

Akizungumza nje ya mahakama hiyo, wakili wa washtakiwa hao, Eric Mutta alisema washtakiwa hao watano bado wameendelea na msimamo wa kutokubali dhamana. "Hawa washtakiwa bado hawajakubali sasa na mimi kama wakili wao siwezi kuwalazimisha wakubali, tunaendelea kuwashauri na siku wakikubali watadhaminiwa maana dhamana zao zipo wazi," alisema Mutta.

Mfalme Zumaridi anakabiliwa na kesi ya kusafirisha binadamu ambayo haina dhamana na kumfanya abaki mahabusu katika gereza la Butimba mkoani Mwanza katika kipindi chote tangu mwishoni mwa mwezi Februari mwaka huu, alipokamatwa pamoja na wafuasi wake.

Kwa mara ya kwanza Machi 3, mwaka huu, wafuasi 92 pamoja na Zumaridi walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza na kusomewa mashtaka matatu. Mashtaka hayo ni pamoja na kushambulia polisi, kuzuia polisi kufanya kazi yao na kusafirisha binadamu ambalo linamkabili Zumaridi peke yake.

Siku ya kwanza mfuasi mmoja alikubali kudhaminiwa na kubaki 91 waliokataa dhamana licha ya kuwa ilikuwa wazi.

Wafuasi hao walidai wapo tayari kwenda Gereza la Butimba mkoani Mwanza pamoja na Zumaridi na kwamba hawatakubali kupewa dhamana na kumuacha peke yake. Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani Machi 3, mwaka huu, ikiwa ni takribani siku saba tangu walipokamatwa nyumbani kwa mchungaji huyo eneo la Buhongwa jijini Mwanza.

Mchungaji huyo ambaye ana wafuasi wengi katika kanisa lake jijini Mwanza, jana alionekana mahakamani hapo akiwa na furaha na hakujifunika uso wake kama ilivyokuwa kipindi cha wiki zilizopita alipofikishwa mahakamani hapo akiwa amejifunika 'gubigubi' kwa kitenge.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Emanuel Luvinga, alidai mahakamani hapo kuwa walijiandaa kuwasomea maelezo ya awali washtakiwa hao, lakini hakimu wao amepata udhuru.

Kutokana na hali hiyo, Wakili huyo aliomba ipangwe siku nyingine ili washtakiwa waweze kusomewa maelezo ya awali.

Katika kesi hiyo, Zumaridi alinyimwa dhamana kwa kuwa kosa la usafirishaji binadamu halina dhamana kwa mujibu wa sheria. Wakili Luvinga alieleza mahakama hiyo kwamba, kesi namba 10 ya mwaka 2022 inamhusu mchungaji Diana Bundala na wenzake wanane ambao wanadaiwa kufanya shambulio la kuzuru mwili na kuzuia maofisa wa polisi kufanya kazi.

Aidha, alisema kesi namba 11 ya mwaka 2022, inamhusu Mfalme Zumaridi, peke yake ambayo ni usafirishaji haramu wa binadamu na kesi namba 12 ya mwaka 2022 inamhusu Zumaridi na wenzake 84 wanaodaiwa kufanya kusanyiko lisilo halali.

## ... Watumishi walivyolipana posho za mabilioni bila kodi

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kulipa posho za Sh. bilioni 61.64 kwa wafanyakazi wake pasi na kutoza kodi.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Jumanne, CAG Charles Kichere anasema amebaini shirika hilo kutotoza kodi ya Sh. bilioni 17.4 kwenye posho za watumishi.

Anafafanua kuwa Kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2019) kinasema mapato ya mtu binafsi kutokana na ajira kwa mwaka wa mapato yatakuwa faida aipatayo mtu huyo kutokana na ajira ya mtu huyo kwa mwaka wa mapato.

Vilevile, CAG anasema Kifungu cha 7(3)(k) cha sheria hiyo kinaeleza kuwa katika kukokotoa faida aipatayo mtu binafsi kutokana na ajira, posho ambazo hazijumuishwi (posho zisizo za kodi) ni posho ya nyumba, posho ya usafiri, posho ya uwajibikaji, posho ya kazi ya ziada, posho ya muda wa ziada, posho ya mazingira magumu na honoraria kwa mtumishi wa serikali au taasisi ambazo zinalipwa kutokana na bajeti ya vyanzo vingine vya mapato, yaani bajeti isiyotokana na ruzuku kutoka serikalini.

"Hata hivyo, nilipopitia makato ya kodi ya mishahara kwa watumishi wa kudumu, watumishi wa mkataba na watumishi wa muda kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2021, nilibaini posho za wafanyakazi zenye jumla ya Sh. bilioni 61.64 hazikukatwa kodi (Sh. bilioni 53.57 kwa wafanyakazi wa kudumu na Sh. bilioni 8.07 kwa watumishi wa muda) ambazo ni faida kwa wafanyakazi.

"Hali hii ni kinyume cha Sheria ya Kodi ya Mapato kama ilivyoelezwa hapo juu, hivyo kusababisha kutopelekwa kodi ya Sh. bilioni 17.4 katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Sh. bilioni 15.5 kwa wafanyakazi wa kudumu na Sh. bilioni 1.9 kwa wafanyakazi wa muda.

"Hali hii inaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama kwa shirika na faini inayoweza kutolewa na TRA kwa kutowasilisha makato ya kodi kwenye posho za wafanyakazi.

"Ninapendekeza TANESCO ihakikishe kuwa posho zote wanazostahili kulipwa watumishi zinatozwa kodi husika kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, (kama ilivyorekebishwa mwaka 2019)," CAG anasema.

HABARI KITAIFA

# Mikoa mitatu kukosa umeme

Na Idda Mushi, MOROGORO

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limesema mikoa ya Pwani, Tanga na Morogoro itakabiliwa na upungufu wa umeme kutokana na kulipuka moto kituo cha kupooza na kusambaza nishati hiyo cha Msamvu, mjini Morogoro.

Msemaji wa TANESCO, Martin Mwambene, akizungumza na Nipashe kwa simu, alisema kituo hicho kililipuka Aprili 13, mwaka huu, majira ya saa nane mchana, kwenye transfoma mpya iliyofungwa mwaka jana na kuteketeza chumba chenye mitambo ya kusambaza umeme, ikiwa ni mara ya tatu kwa tukio la moto kujitokeza katika eneo hilo.

Alisema kuungua kwa transfoma hiyo kumesababisha wakazi wa mikoa ya Pwani na Tanga wanaotumia kituo cha umeme cha Chalinze, kupata usumbufu kutokana na kupungua ambao sasa wananchi wa Morogoro nao wanalazimika kuutumia.

Kwa mujibu wa msemaji huyo, mafundi wanaendelea na kazi tangu kutokea kwa hitilafu hiyo, na kwamba lengo ni kurudisha umeme kadri itakavyowezekana ndani ya kipindi kifupi.

"Kwa sasa sio rahisi kujua hasara iliyopatikana au kuendelea kupatikana, lakini tutatoa tathmini ya hasara iliyotokea baada ya kazi kukamilika," alisema Mwambene.

Alibainisha kuwa kikubwa wanachoangalia ni kuhakikisha wananchi wa Morogoro hawakosi huduma ya umeme na ndiyo maana wametafuta njia mbadala ya kutumia kituo cha Chalinze.

"Mafundi walitarajia ingechukua siku moja kukamilika, lakini hali imekuwa tofauti na mafundi bado wapo kazini usiku na mchana ili tatizo hili litatuliwe," aliongeza. Jana, Meneja wa TANESCO Mkoa wa Morogoro, Mhandishi Fedgrace Chuma, alisema moto huo ulitokea wakati mafundi wakifanya marekebisho ya kawaida kwenye mitambo ya kituo hicho cha kupooza na kusambaza umeme cha Msamvu.



Mjumbe wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani, Ibrahim Gama (kushoto), akila kiapo cha kushika nafasi hiyo, mbele ya Mkuu wa mkoa huo, Abubakari Kunenge, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waziri Mkuu India anavyomkumbuka Mwalimu Nyerere

Na Romana Mallya

WAKATI Taifa likiadhimisha miaka 100 ya kuzaliwa kwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi, amesema maisha na kazi zake zitabaki kuwa hamasa kwa watu wote.

Modi kupitia ukurasa wake wa mtandao wa Twitter juzi ikiwa ni siku 100 tangu kuzaliwa kwa Mwalimu Nyerere, aliandika kuwa, umoja na usawa alioutengeneza kiongozi huyo bado unaendelea kuakisi maisha ya sasa.

Modi alisema: "Maisha ya Mwalimu Nyerere na kazi zake zitabaki kuwa hamasa katika maisha ya sasa."

Modi amedumu nafasi ya uwaziri mkuu wa India kwa miaka 14 tangu mwaka 2014, pia alikuwa Waziri Mkuu wa Gujarat kutoka mwaka 2001 hadi 2014 na ni mbunge wa Bunge la Taifa kwa Jimbo la Varanasi.

Katika ukurasa wake, Modi pia alisema katika kuadhimisha miaka 100 ya kuzaliwa kwa muasisi huyo wa Taifa la Tanzania huo ndiyo ujumbe wake kwa kiongozi huyo ambaye alikuwa rafiki wa karibu wa Taifa la India.

Mwaka 2016, Modi alikuja Tanzania kwa ziara ya siku moja na kutembelea barani Afrika kwa lengo la kukuza

# Bil. 14/- kugharimu uanzishaji mfumo jumuishi kielektroniki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema Sh. bilioni 13.8 zinahitajika kugharamia uanzishaji wa mfumo jumuishi wa kielektroniki wa huduma za ustawi wa jamii nchini.

Mfumo huo unalenga kusaidia upatikanaji wa takwimu za watoto walio katika mazingira hatarishi na kutoa taarifa kwa watoto waliofanyiwa ukatili na wanao kinzana na sheria.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua kikao cha wadau cha kuanzisha mfumo huo, jijini hapa.

Alisema fedha hizo ni kwa ajili ya kusanifu, kutengeneza hadidu za rejea, miundombinu, kuandaa wataalamu wa kutumia mfumo na kusambaza mfumo huo jumuishi nchi nzima.

"Mashirika ya maendeleo na wadau wote mnaombwa kuunga mkono juhudi za serikali moja kwa moja kwa kuelekeza rasilimali fedha na ujuzi katika eneo hili ili kuanzisha mfumo jumuishi wa huduma za ustawi wa jamii ili kuboresha utoaji huduma," alisema.

Alisema mfumo huo utasaidia upatikanaji wa takwimu za biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu, msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa ukatili, madawa ya kulevya, ulinzi na usalama kwa makundi maalum.

"Mfumo unaopendekezwa utasaidia kupata takwimu za huduma katika vituo vya kutolea huduma kama vile makazi ya wazee, nyumba salama, vituo vya mkono kwa mkono, vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na makao ya watoto," alisema.

Naye, Kaimu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mwajuma Magwiza, alisema mwaka 2017 serikali ilipata msaada wa kifedha kutoka Shirika la Kimataifa la Watu wa Marekani (USAID), Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na wadau wa maendeleo ikiwamo Measure evaluation na PACT kwa ajili ya kutengeneza mifumo kusajili mashauri ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi kwa kukusanya kwa mtu mmoja mmoja (DCMS) na taarifa zilizojumuishwa (MVC-MIS).

Hata hivyo, alisema kuna vikwazo mbalimbali ikiwamo mfumo wa MVC-MIS kukosa uwezo wa kufuatilia usimamizi wa shauri kwa mtoto mmoja mmoja.

"Kukosekana kwa uwezo wa kufuatilia taarifa hizo kwa mtoto mmoja mmoja inazuia Wizara pamoja na wadau kutumia mfumo huo kutengeneza afua zinazomlenga mnufaika," alisema.

Kwa upande wake, Mtaalamu wa Mifumo kutoka USAID, Edwin Nyella na Mtaalamu wa Ulinzi wa Watoto kutoka UNICEF, Evance Mori, waliahidi kuunga mkono serikali katika usimikaji wa mfumo huo na uboreshaji wa mifumo iliyopo ya taarifa hizo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali isikubali nauli kupandishwa kiholela

**KIPINDI** hiki ambacho ulimwengu unakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwamo kupanda kwa bei ya mafuta na bidhaa, kimesababisha baadhi ya wafanyabiashara kuanza kupandisha bei za bidhaa na gharama za huduma.

Kupanda kwa bei ya mafuta na baadhi ya bidhaa kumechangiwa na vita vinavyoendelea kati ya Russia na Ukraine, ambazo ni wazalishaji wa mafuta na bidhaa nyingine, ikiwamo ngano.

Serikali imekuwa ikitoa taarifa kuhusiana na hali hiyo ngumu ya uchumi, huku ikitaja hatua mbalimbali inazojaribu kuzichukua kuhakikisha kwamba wananchi wanapunguziwa makali hayo.

Kadhalika, imekuwa ikitoa angalizo kwa wafanyabiashara kutopandisha bei ya bidhaa na huduma kiholela kinyume cha uhalisia, ingawa inashuhudiwa baadhi wakiendelea kuitumia fursa hiyo kupandisha bei.

Ni kweli kwamba kupanda kwa bei ya mafuta kunaathiri baadhi ya bidhaa, lakini hatukubaliani kabisa na baadhi ya bidhaa kupandishwa bei kwa kisingizio cha bei ya mafuta, kwa sababu hazihusiani kabisa na mafuta.

Hivi sasa kuna shinikizo kubwa kutoka kwa wasafirishaji wa abiria kwa maana ya mabasi ya daladala na mabasi yanayokwenda mikoani kutaka kupandishwa bei ya nauli kutokana na sababu hiyo hiyo, ingawa mapendekezo yao ya viwango vya nauli wanayopendekeza hayana uhalisia na hali halisi.

Mapendekezo ya viwango vya nauli yaliyotolewa juzi wakati wa mkutano wa wadau wa usafirishaji na serikali uliofanyika jijini Dar es Salaam ni uthibitisho kwamba hayakufanyiwa utafiti wa kina kabla ya kuyawasilisha hadharani.

Tunasema hivyo kwa sababu viwango vya kauli wanavyovipendekeza vikikubaliwa, wananchi wengi watashindwa kuvimudu kutokana na hali halisi ya uchumi na vipato vyao.

Katika mkutano huo wa wadau hao waliiomba serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kupandisha bei za usafiri wa daladala na mabasi ya kwenda mikoani kwa maelezo kuwa gharama za maisha zimepanda.

Wanapendekeza nauli kuongezaka kwa asilimia 34 hadi 54 kwa mikoani, huku kwa mijini kilometa 10 iwe Sh. 745.00, kilometa 15 (Sh. 1,117.40), kilometa 20 (Sh. 1,490), kilometa 25 (Sh. 1862.50) na kilomita 30 (Sh. 2235).

Chama cha Wamiliki wa Mabasi nchini (TABOA), kinasema nauli za mabasi yaendayo mikoani zinazotumika kwa sasa zina zaidi ya miaka tisa wakati gharama za vyombo vya usafiri, ilikuwa ndogo, hivyo kuna haja ya kuzibadilisha kwa kuwa sasa zimepanda.

Kwamba imekuwa chini kwa muda mrefu kwa sababu mara ya mwisho nauli zilirekebishwa mwaka 2013, na kwamba gharama za maisha zimepanda ukilinganisha miaka hiyo na sasa. Inasema kipindi hicho dola moja ilikuwa ni sawa na Sh.1,596 wakati leo hii dola moja ni Sh. 2,345.

Sababu nyingine TABOA inadai gharama za kununulia mabasi nazo zimepanda ukilinganisha na kipindi cha nyuma hadi kufikia Sh. miioni 400 kutoka Sh. milioni 200 kwa mabasi yanayotoka China huku kwa Marcopolo zimepanda hadi Sh. milioni 700, hivyo kuziomba mamlaka kupandisha ili kuendana na kasi hiyo.

Wamiliki wa Daladala Dar es Salaam (DARCOBOA), wanadai kwa umbali wa kilometa 10 nauli iwe Sh. 745.00, kilometa 15 (Sh. 1,117.40), kilometa 20 (Sh. 1,490), kilometa 25 (Sh. 1,862.50), kilomita 30 (Sh. 2,235), huku wakipendekeza wanafunzi walipie nusu ya gharama hizo.

Hata hivyo, Chama cha Kutetea haki za Abiria Taifa (CHAKUA), kilieleza kuwa wakati wadau wa usafiri wanajadili kupandishwa nauli wafirikirie pia suala la kuboresha utoaji wa huduma hizo kwa sababu kwa sasa sio nzuri.


Kilisema watu wanakata ruti, sehemu ya nauli ya chini wanapandisha, ya nauli ya juu wanapunguza hawaeleweki, na kusisitiza abiria na watoa huduma kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria.

Kimsingi, viwango vilivyopendekezwa ni vikubwa mno, visivyozingatia uhalisi wa hali za wananchi na hivyo tunaishauri kama itaona kuna sababu za msingi, ipandishe nauli mpya kwa kuzingatia uhalisia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Tunafanyia masihara hatari ya kuziba meno tukitumia zebaki



Na Yasmine Protace

**UGONJWA** wa kuumwa jino, unaweza kumpata mtu yoyote na ikapelekea kulitoa au kuliziba.

Mtu anayesumbuliwa na jino, anapoenda hospitali kupata matibabu, kwanza litaangaliwa na wataalamu wa meno na kisha wanamshauri kitu ambacho atafanyiwa, ili asiendelee kupata maumivu.

Yupo mtu ambaye jino linamsumbua na anapofika kwa wataalamu wa meno, anapochekiwa watampa ushauri kama watalitoa, wataliziba au watamsafisha.

Ni majibu yanayotolewa na wataalamu wa meno na sio chaguo la mgonjwa. Pengine tu, mgonjwa huyo anaweza kushirikishwa katika uamuzi, kupata muafaka ulio bora zaidi kitaalamu.

Ukiangalia kwa sasa, maeneo ya huduma za meno ni mengi, pia hata katika fremu ambazo watu wamezikodisha, nao wameweka mabango yao kuwa wanatoa huduma za meno.

Mtu ukipita hata katika baadhi ya barabara zenye watu wengi, utakuta matangazo kupitia katika magari yakisema wanatoa huduma za meno pasipo kung'olewa.

Sasa hao wanaojitangaza kukupatia huduma za meno bila ya kukung'oa wana elimu juu ya athari za kuziba meno kwa kutumia madini ya zebaki na madini mengineyo, wana maana gani?.

Hivi karibuni Wizara ya Afya kwa kushirikiana na asasi ya Agenda, walitoa tamko kuwataka wataalamu wa Afya ya kinywa na meno kutokuziba meno, bila ya kutumia dawa yenye madini ya zebaki ijulikanayo kama Amalgma, kutokana na kuwa na athari kwa binadamu.

Wito huo umetolewa na Ofisa kutoka Idara ya Tiba, katika Wizara ya Afya, Dk. Msafiri Kabulwa wakati wa mafunzo kwa wataalamu wa afya ya kinywa na meno, akijadili kuziba meno kwa kutumia kemikali zisizo na madini ya zebaki, yaliyofanyika jijini Mbeya.

> **"Zebaki huweza kutoka kwa mama mjamzito na kuingia kwa mtoto aliye tumboni wakati wa ujauzito, ama kupitia maziwa ya mama wakati wa kunyonyesha na kuleta athari katika ukuaji wa ubongo wa mtoto," anasema Dk. Msafiri**

Dk. Msafiri anasema madini ya zebaki yana athari kubwa kwenye mazingira na afya ya binadamu, pia ina uwezo wa kuharibu ukuaji wa ubongo wa mtoto tangu akiwa tumboni kwa mama.

"Zebaki huweza kutoka kwa mama mjamzito na kuingia kwa mtoto aliye tumboni wakati wa ujauzito, ama kupitia maziwa ya mama wakati wa kunyonyesha na kuleta athari katika ukuaji wa ubongo wa mtoto," anasema Dk. Msafiri

"Athari za ukuaji wa ubongo ni pamoja na kuharibu uwezo wa mtoto wa kufikiri na hatimaye kumfanya mtoto ashindwe kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya kiuchumi hapo baadaye," anafafanua.

Anasema wizara hiyo imelenga kuikinga jamii dhidi ya madhara yatokanayo na madini ya zebaki kwa kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kuzibia meno zisizokuwa na madini ya zebaki kupitia bohari ya dawa(MSD)

Kemikali za kuzibia meno zisizokuwa na madini ya zebaki zinapatikana hapa nchini kwa wasambazaji binafsi na kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

Nilipenda hata hoja ya Ofisa Programu Mwandamizi wa asasi ya Agenda Dorah Swai, akisema mwaka 2013, Tanzania iliungana na nchi nyinginezo duniani kutia saini mkataba wa kimataifa wenye lengo la kulinda afya na mazingira, kutokana na athari za zebaki.

Anautaja unajulikana Mkataba wa Minamata wa Zebaki ambao Tanzania iliridhia mkataba huo mwezi Oktoba 2019, hivyo kuna hitaji kuuzidishia nguvu ya utekelezwaji wake hapa nchini.

"Kwa sasa ni juu ya wataalamu wetu kuunga mkono juhudi hizo kwa kutimiza yale yote yaliyoainishwa kwenye mwongozo na kwenye kanuni, endapo walikuwa hawajaanza kufanya hivyo," anasisitiza Dorah

HABARI KITAIFA

# Machinjio Shinyanga yakabiliwa upungufu mifugo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MACHINJIO ya mifugo ya kisasa Manispaa ya Shinyanga mkoani hapa, inakabiliwa na upungufu wa mifugo ya kuchinja tofauti na matarajio.

Machinjio hayo yalianza rasmi kazi ya uchinjaji mifugo Novemba mwaka jana, na ilitarajiwa kuchinja ng'ombe 500 na mbuzi 1,000 kwa siku, lakini kwa sasa wanachinjwa g'ombe 38 na mbuzi 40.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, John Tesha, alibainisha hayo jana wakati akisoma taarifa ya machinjio hayo kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alipotembelea maendeleo yake.

Tesha alisema malengo mahususi ya machinjio hayo ni kuongeza thamani ya mazao ya mifugo katika mnyororo wa thamani wa nyama na kuongeza mapato kwa wadau wote wa mifugo na serikali, lakini tatizo ambalo linawakabili ni upungufu wa mifugo.

"Machinjio hii ya kisasa imejengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 5.1 na matarajio ilikuwa ni kuchinja ng'ombe 500 na mbuzi 1,000 kwa siku, lakini hali ni tofauti hakuna mifugo, tunachinja chini ya lengo," alisema Tesha.

Alisema, mikakati iliyopo ni kutafuta wawekezaji wanaofanya biashara ya kusafirisha nyama nje ya nchi ili watumie machinjio hayo na kufikia lengo halisi la uchinjaji kwa siku.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki, aliagiza machinjio hayo yanapaswa kutangazwa zaidi katika mikoa ya jirani ili itambulike na wafugaji kupeleka mifugo yao na kufikia malengo.

Vile vile, alisema wizara watakwenda kulifanyia kazi suala la kutafuta mwekezaji kwenye machinjio hayo, ambaye pia atakuwa akiuza nyama ndani na nje ya nchi na kufikia malengo yaliyokusudiwa ya ujenzi wa machinjio.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Mashimba Ndaki (wapili kushoto), akiangalia mitambo katika machinjio ya kisasa ya Manispaa ya Shinyanga, alipofanya ziara ya kikazi jana. Kushoto ni Mkaguzi Mkuu wa Machinjio hiyo, Ernest Nigo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Viongozi wa dini waombwa kukemea ukatili

**Na Romana Mallya**

BAADA ya kushamiri vitendo vya unyanyasaji na ukatili vilivyosababisha mauaji na majeruhi ndani ya jamii, Jeshi la Polisi nchini limewaomba viongozi wa dini wasaidie kuvikemea.

Kwa mujibu wa taarifa yao iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi hilo, David Misime, jeshi hilo pia limewaomba waumini na Watanzania kwa ujumla kuelimishana, kukemea maovu ndani ya familia. "Tunaomba muendelee kuelimishana na kukemea maovu ndani ya familia na jamii kuhusu unyanyasaji na ukatili unaosababisha mauaji, majeruhi, kubaka na kulawiti," alisema. Pia, aliomba waendelee kukemea uzembe na ukaidi wa baadhi ya waendesha vyombo vya moto wa kutofuata sheria za usalama barabarani unaosababisha ajali, vifo, uharibifu wa mali na kuacha watoto yatima.

Kuhusu ibada za kuelekea Sikukuu ya Pasaka, Misime alisema wamejiimarisha kwa kushirikiana na viongozi wa dini hususan kamati za ulinzi katika makanisa kuhakikisha amani, utulivu na usalama unaimarishwa.

Kadhalika, alisema ushirikiano wanaopata kutoka kwa wananchi umewezesha kupata mafanikio katika doria, misako na operesheni zao na kuifanya nchi kuendelea kuwa shwari.

# Hospitali Chato yakumbwa uhaba mkubwa wa dawa

**Na Daniel Limbe,** CHATO

HOSPITALI ya Wilaya ya Chato mkoani Geita, inakabiliwa na uhaba wa dawa hali inayotishia baadhi ya wagonjwa kupoteza maisha.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wagonjwa na ndugu katika hospitali hiyo, wamesema wanalazimika kutumia fedha nyingi kupata matibabu kutokana na kutakiwa kununua dawa kwenye maduka ya watu binafsi.

Gelard Nyambele, mkazi wa kijiji cha Kanyama, alisema ndugu yake ambaye ni mgonjwa amefanyiwa upasuaji mkubwa wa kuondoa bandama tumboni, lakini dawa nyingi aliagizwa kununua kwenye duka la serikali lililopo kwenye maeneo ya hospitali hiyo.

"Tuliambiwa ili kumsaidia mgonjwa wetu tunapaswa kuwa na fedha za kununulia dawa zinazohitajika kwa kuwa hospitali hiyo haina dawa zinazofaa kwa ajili ya mgonjwa wetu," alisema Nyambele.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini kutokuwapo kwa baadhi ya dawa muhimu zaidi ya miezi sita ikiwamo 'panadol' hali inayowakatisha tamaa baadhi ya wagonjwa na kulazimika kutafuta huduma vituo binafsi vya afya na wengine kutibiwa kwa waganga wa jadi.

Aidha, hali hiyo imechangia kushuka kwa mapato yatokanayo na uchangiaji huduma kutokidhi kiwango cha kuagiza dawa hizo kutoka Bohari ya Dawa Nchini (MSD) na kusubiri kudra za dawa zilizolipiwa kupitia ruzuku ya serikali kuu.

Uchunguzi umebaini pia mapato yameshuka kwenye hospitali hiyo kutokana na baadhi ya makundi kutotakiwa kuchangia huduma hizo ikiwamo wajawazito, watoto chini ya miaka mitano na wazee zaidi ya miaka 60.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Chato, Dk. David Mudeba, alikiri kuwapo kwa uhaba wa dawa muhimu kwenye hospitali hiyo na kudai kuwa tatizo hilo ni la kitaifa.

"Ni kweli tuna tatizo la uhaba wa baadhi ya dawa...hii inatokana na matatizo ya kimfumo MSD ndiyo wanapaswa kutusambazia huduma hiyo...fedha zetu nyingi zipo kwao ndiyo maana hata Rais Samia Suluhu, ameamua kupangua pale MSD ili kuboresha huduma," alisema Dk. Mudeba.

Uhaba wa dawa umekuja ikiwa ni siku chache tangu baadhi ya wajawazito kulalamika mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule, kwamba wanatozwa fedha na vifaa vingine wanapokwenda kujifungua kwenye hospitali hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Christian Manuga, alipotakiwa kuelezea tatizo hilo, alisema hana taarifa hizo huku akiahidi kuambatana na Mganga Mkuu wa wilaya hiyo kwenda kujiridhisha kabla ya kutoa majibu kwa vyombo vya habari.

# Binadamu walivyoathiri Shoroba ya Kwakuchinja

**Na Salome Kitomari**

ONGEZEKO la watu, shughuli za kibinadamu, kukosekana mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji na ujangili wa kitowewo ni changamoto kubwa zinazolikabili eneo la mapito ya wanyamapori ya Kwakuchinja, lililopo wilayani Babati Vijijini mkoani Manyara.

Hali hiyo imesababisha usumbufu kwa wanyama kulazimika kubadilisha muundo wa maisha, huku zikihitajika jitihada za wadau wote kuhakikisha wanyama wanakuwapo na binadamu.

Akiwasilisha mada ya ushiriki wa sekta binafsi kwenye uhifadhi kwa waandishi wa habari kwenye mkutano mtandaoni ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) kwenye mradi wa kuhifadhi maliasili unaofadhiliwa na Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Kaimu Mkurugenzi wa Chemchem, Walter Palangyo, alisema ushirikiano na jamii umesaidia kuendeleza uhifadhi.

Alisema changamoto nyingine ni wanyama kugongwa na magari, na kwamba wastani wa aina 50 hufa kwa mwaka, huku kwa siku si chini ya tatu.

Pallangyo alisema hali hiyo inatokana na uzembe wa madereva kutozingatia alama za barabarani ambazo zinaonyesha kuwa eneo hilo ni mapito ya wanyamapori, na kwamba ni lazima kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria ili kuokoa wanyama hao kupotea.

"Tunaona watu wameongezeka ambao wanatumia wanyamapori kwa ajili ya kitowewo, kuongeza maeneo ya kilimo, kukata miti hadi kwenye mpaka wa hifadhi au mapito na kutozingatia kuacha mita 500 kutoka mpakani, hali inayoongeza migogoro baina ya wanyama pori na binadamu.

Alisema Chemchem imekuwapo eneo hilo lenye Hifadhi ya Jamii ya Burunge, Mapito ya Wanyamapori na Hifadhi za Taifa za Tarangire na Ziwa Manyara tangu mwaka 2016. "Ilianzishwa kwa ajili ya kuweka usawa wa uhifadhi na shughuli za binadamu, wamekuwa wakisaidia jamii kutekeleza shughuli zake kwa lengo la kulinda maliasili, tumesaidia miradi mingi ya kijamii ikiwamo kuviwezesha vikosi vya ulinzi, huku wakitoa zawadi kwa watoa taarifa za kusaidia kukabili ujangili," alisema.

"Tumetengeneza vikundi vya kinamama ambao wanaweka akiba na kukopeshana kwenye vikoba ambayo inawasaidia kuwekeza kwenye shughuli nyingine ambazo ni rafiki kwa mazingira ikiwa ni utaratibu uliowekwa, pia tunawaongezea mtaji ili wasiwe na tamaa ya kuingia kwenye shughuli hasi za uhifadhi," alisema.

"Tulitoa basi maalum kubeba wanafunzi kutoka kijiji cha Vilima vitatu hadi Minjingu ambao ilikuwa lazima kila siku alfajiri wapitie kwenye shoroba umbali wa kilomita 15 wanakutana na wanyama wakali, tumegawa viti mwendo 120 lengo jamii ione umuhimu wa kuwa karibu na hifadhi," alisema.

Kwa mujibu wa Pallangyo, katika kukabiliana na tembo waharibifu walifunga kamera eneo hilo, kuwapa simu na tochi ili kutoa taarifa za uwepo wa wanyama ambao wanafukuzwa kabla ya kuleta uharibifu, huku wakiimarisha maboma 19 ya wanyama vijiji vya Sangiwe na Vilimavitatu.

Naye, Mchambuzi wa sera wa TPSF, Victoria Michael, alisema kwenye utalii na uhifadhi wanawachama wao huangalia changamoto wanazokutana nazo wafanyabiashara, wawekezaji kwenye maeneo ya maliasili ambazo ni sera, matumizi ya ardhi ambazo huwasilishwa na kujadiliwa katika ngazi mbalimbali ili kupata ufumbuzi.

"Tulikuwa na mradi wa kukuza uelewa wa kutunza maliasili kwa sekta binafsi, kwa kuwa ujangili na uharibifu wa mazingira haziwezi kufanywa na serikali pekee kwa kuwa nyingi zinafanywa na sekta binafsi, tuliwaelimisha wajibu wao katika kupunguza changamoto," alisema. Alisema walifikia zaidi ya kampuni 190 za sekta zote, mfano msafirishaji amebeba mzigo hajui ni mzigo gani kumbe amebeba meno ya tembo, ambao tuliwafundisha wadau kwenye viwanja vya ndege, ili watambue bidhaa za wanyamapori wasipitishe.

# Magari yatozwa faini kwa kuzidisha uzito

**Na Joctan Ngelly**, GEITA

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Geita, umekamata magari 35 kwa madai ya kuzidisha uzito barabarani katika upimaji wa magari 1,184 uliofanyika kwa muda wa wiki mbili kwa kutumia mizani inayohamishika katika maeneo ya Geita mjini na Katoro.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Geita, Japherson Michael, alisema jana ofisini kwake kuwa baada ya kugundulika kuwa yamezidisha uzito, magari hayo yalipelekwa kwenye mizani ya kudumu iliyoko Usagara, Mwanza na Bwanga wilaya ya Chato ndipo magari sita kati ya 35 yakathibitika kuwa yamezidisha uzito na mengine 29 yaliruhusiwa na kuendelea na safari.

Alisema magari hayo sita yalitozwa faini ya Sh. milioni mbili na kulipa kabla ya kuruhusiwa kuondoka.

Pamoja na kufanya hivyo, meneja huyo alisema mkoa unakabiliwa na ukosefu wa maeneo mazuri yenye nafasi ya kutosha kwa ajili ya upimaji wa magari, hivyo kulazimika kufanya kazi hiyo kuwa ngumu.

Alisema ili kukabiliana na changamoto hiyo, wataboresha baadhi ya maeneo ya barabara husika ili kurahisisha utekelezaji wa kazi hiyo siku zijazo.

Michael alitaja changamoto nyingine kuwa ni madereva kutopenda uwapo wa mizani barabarani.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa lengo kuu la kuweka mizani inayohamishika ni kuhakikisha magari yanayopita barabarani hayazidishi uzito kwa kutambua kuwa wakati wowote yanaweza kubainika.

Aliwataka madereva kuzingatia elimu wanayopewa na wafanyakazi wa mizani kuhusu kubeba uzito unaokubalika na kutii maelekezo wanayopewa wakati wa zoezi la upimaji magari.

Meneja huyo alisema upimaji magari kwa kutumia mizani inayohamishika utakuwa endelevu kwa mkoa wa Geita ili kuhakikisha magari yote yanayopita barabarani hayazidishi uzito.




Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Ardhi (ARU), Prof. Evaristo Liwa (kushoto) na Balozi wa Ubelgiji nchini, Peter Van Acker, wakizindua kwa pamoja kituo cha Utafiti na Mafunzo, chuoni hapo, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TBS yawahamasisha wajasiriamali kuchangamkia fursa kupima bidhaa

**Na Joseph Mwendapole**

WAJASIRIAMALI nchini wametakiwa kuchangamkia fursa ya kuthibitisha ubora wa bidhaa zao bure inayotolewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili kushiriki kikamilifu kwenye uanzishaji wa viwanda.

Wito huo ulitolewa jana na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa TBS, Viola Masako, ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu, Dk. Yusuf Ngenya, wakati wa hafla ya kukabidhi vyeti na leseni kwa wazalishaji ambao bidhaa zao zimethibitishwa na kukidhi viwango.

Katika hafla hiyo, TBS ilitoa vyeti na leseni 211 na kati yao 115 sawa na asilimia 55 ni wajasiriamali wadogo ambao wamethibitishiwa bidhaa zao kwa kipindi cha Januari na Machi, mwaka huu.

Masako alisema walitoa leseni 96 sawa na asilimia 45 za wazalishaji wengine wanaohusika na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwamo za vyakula, vipodozi, viatu, vifaa vya ujenzi, umeme, magodoro na vifungashio.

"Kwa kweli nawapongeza sana kwa mafanikio haya pamoja na serikali kuendelea kulipia gharama za upimaji wa bidhaa za wajasiriamali wadogo na wa kati katika ukaguzi na upimaji wa bidhaa zenu na hiki ni kielelezo kwamba Rais wetu ana imani kubwa sana na shirika letu la TBS," alisema.

Katika kuunga mkono jitihada za serikali za kuimarisha uchumi, alisema TBS imeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuwahudumia wajasiriamali kupata alama ya ubora.

"Na mchakato wote wa ukaguzi, upimaji hadi kupata vyeti na leseni ya kutumia alama ya ubora kwa wajasiriamali ni bure kabisa na ninyi nyote ni mashahidi wa jambo hili," alisema.

"Kwa mwaka huu wa fedha, TBS imetenga Sh. milioni 256 kwa ajili ya kuwahudumia wajasiriamali, hivyo tunatoa wito kwa wajasiriamali katika mikoa yote kuchangamkia fursa hii iliyotolewa na Serikali kwa ajili ya kuanzisha viwanda ambavyo vitaweza kutengeneza ajira kwa Watanzania," aliongeza.

Alisisitiza kuwa wazalishaji hao wakianzisha viwanda ana imani watazalisha ajira na uchumi utakua.

Kwa mujibu wa Masako, serikali inatambua kwamba bidhaa zilizothibitishwa ubora ni salama, hivyo alitoa wito kwa waandishi wa habari nchini kuendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kutumia bidhaa zilizothiitishwa ubora na TBS kwa sababu lengo kuu ni kuhakikisha wanalinda afya za walaji.

Alisema wazalishaji ambao wamethibitisha bidhaa zao wanakuwa na fursa ya kupanua masoko ya bidhaa zao bila vikwazo.

"Kwa hiyo tunatoa rai mfuate taratibu kuthibitisha bidhaa zenu, kwani mkifanya hivyo mtaepuka hasara ambazo zinaweza kujitokeza na pia mtalinda afya za walaji," alisema.

## Sekta ya kilimo yahakikishiwa uwezeshwaji

**Na Mwandishi Wetu**

Sekta ya kilimo imehakikishiwa kuendelea kuwezeshwa ili kufikia malengo.

Ahadi hiyo imetolewa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kwa kueleza kuwa itaendeleza malengo yake kwa kuongeza tija kwenye kilimo kwa kutoa fursa zaidi kwa wanafunzi wa vyuo ili kutekeleza azma hiyo kwa vitendo kupitia programu yao ya kilimo na viwanda.

Kwa mujibu wa SBL, wamedhamiria kuwaandaa wanafunzi wa vyuo kujiajiri wenyewe katika fani ya kilimo baada ya kuhitimu kozi zao za stashahada ikiwa pia miongoni mwa nguzo zao za kujenga jamii endelevu ifikapo mwaka 2030 kupitia fursa sawa na jumuishi za elimu, ujuzi, rasilimali ili kujenga jumuiya shirikishi ambapo kila mtu atanufaika.

Akizungumza katika hafla ya kuwatunuku vyeti vya utambulisho waliopata ufadhili huo katika taasisi ya mafunzo ya kilimo Kilacha, Meneja wa Kiwanda cha Moshi, Alice Kilembe, alisema: "SBL inajivunia kuwa na historia ya kuimarisha sekta ya kilimo; tunafanya kazi na mamia ya wakulima nchini Tanzania ambao wao hutuuzia nafaka za kutengeneza bia kama vile mahindi, mtama na shayiri; kwa sababu hiyo, programu hii imeundwa ili kuwatayarisha wanafunzi kuwa wakulima wakubwa na wenye mafanikio katika kilimo biashara."

"Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, programu yetu ya kilimo pia imetoa msaada wa kiufundi na kifedha ambao umechangia maendeleo ya wakulima 400 na jamii zinazowazunguka, na tumeweza kukusanya malighafi hadi tani 18,000 kila mwaka, hivyo kukuza kipato cha wakulima na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa kupitia ulipaji kodi wa mara kwa mara," alifafanua.

Aliongeza kuwa kampuni imeahidi kuendeleza mchango wake kuimarisha kilimo nchini kwa kuanza na vijana vyuoni kupitia mpango wao wa ufadhili wa masomo ujulikanao kama kilimo, viwanda na ufadhili wa masomo, ambao zaidi ya wanafunzi 200 wamenufaika tangu kuanzishwa kwake mnamo mwaka 2019.

Mkuu wa chuo hicho, Benito Mwenda, alipongeza juhudi za SBL katika kuwaelimisha wanafunzi kuhusu ulimwengu wa kilimo cha biashara.

Mwenda alisema mpango huo umeanza kuweka msingi imara kwa wanafunzi.

# Pinda: Kaulimbiu ya wizara itumike kumuenzi Nyerere

**Na Christina Haule, Mara**

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, amesema kauli mbiu ya Wizara ya Maliasili na Utalii 'Tumerithishwa, Tuwarithishe' itumike kwa sababu ina maana hata wakati huu ambao Taifa linaendeleakumuenzi Baba waTaifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Alisema kuna umuhimu wa viongozi waliopo madarakani kuwarithisha vijana mazuri waliyorithishwa kutoka kwa viongozi wengine akiwamo Mwalimu Nyerere, hususan uadilifu na kukataa vitendo vyarushwa na ufisadi.

Pinda aliyasema hayo wilayani Butiama mkoani Mara, kwenye kilele cha maadhimisho ya miaka 100 ya Hayati Mwalimu Nyerere, kwenye banda la maonesho la Wizara ya Maliasili naUtalii, yakiwa na ujumbe: "Tumuenzi kwa kudumisha amani, umoja, uhuru na kazi."

"Tukitazama dhana ya kurithishwa na kurithisha, lazima awamu zote zilizopita na zilizopo, tuyachukue na tuone kuwa ni kitu kinachomhusu mwingine na mwingine kwa manufaa ya wote." alisema.

Akizungumzia suala la malezi, Pinda alisema malezi yana nafasi kubwa ya kumpika kiongozi kuanzia ngazi ya familia hadi katika uongozi wa umma, kama ilivyokuwa kwa Mwalimu Nyerere.

Kuhusu ugonjwa wa Uviko-19, alisema bado upo na kuhimiza watu kujitokeza kupata chanjo,huku akisisitiza watu kuitikia wito kwenye Sensa ya Watu na Makazi, na kwamba kila Mtanzania anawajibu wakuhesabiwa ifikapo Agosti, mwaka huu kwa manufaa yake na nchi kwa ujumla.

Naye, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema wizara imeandaa namna ya kumuenzi Hayati Mwalimu Nyerere kwa kuinua sekta ya utalii nchini .

Alisema katika tathmini iliyofanywa, Wizara imebaini zipo hatua zimechukuliwa katika kuenzi urithiwa Mwalimu Nyerere kwa kuanzishwa makumbusho ya Mwalimu Nyerere.

Naye, Kiongozi Mkuu wa Ukoo waBurito unaolea familia 13,ikiwemo ya Mwalimu Nyerere, Chifu Japhet Wanzagi, alishauri kujengwa sanamu ya Mwalimu Nyerere kwenye mzunguko mmojawapo wa barabara mjini Musoma.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, aliwataka watanzania kuingia kwenye chaguzi zote zijazo na kuchagua viongozi bila rushwa.

Mamlaka ya Usimamizi waWanyamapori Tanzania (TAWA), imeshiriki kikamilifu na kuweka Banda la maonesho katika maadhimisho hayo ya miaka 100 ya Hayati Mwalimu Nyerere, ikiongozwa na Kaimu Naibu Kamishna wa Uhifadhi Sylivester Mushi ambaye alimwakilisha Kaimu Kamishna wa Uhifadhi Mabula Misungwi Nyanda.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa kituo cha kuzalisha gesi asilia cha PanAfrican Energy Tanzania (PAET), James Mughenyi, alipofanya ziara ya kutembelea mradi wa kuzalisha gesi asilia unaoendeshwa na PAET, mkoani Lindi mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bilioni 11 kumaliza kero ya maji Yangeyange, Nzasa na Somelo

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), inatekeleza mradi wa maji Yangeyange ambao umeshika kasi na sasa umefikia hatua ya ulazaji wa mabomba ya kusafirisha maji.

Mradi huo ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia (WM) na kusimamiwa na DAWASA mpaka kukamilika kwake utagharimu Sh bilioni 11.

Mkandarasi wa Mradi huo, Mhandisi Michael Njau, alisema jana kuwa kazi ya uboreshwaji wa kisima cha maji, ujenzi wa matenki ya maji pamoja na ulazaji wa miundombinu ya maji imeanza kutekelezwa.

Alisema pamoja na ulazaji wa mabomba kazi inayoendelea kwa sasa ni ujenzi wa matenki na uboreshaji wa kisima.

Alisema kazi ya ujenzi wa matenki mawili yenye ujazo tofauti tofauti katika eneo la Mgeule na Nzasa imeshaanza na inaendelea kwa kasi kubwa.

"Kazi hii tumeianza na tunatarajia kuitekeleza kwa kipindi cha mwaka mmoja ambapo katika eneo la Mgeule tunajenga tenki la juu lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni moja na katika eneo la Nzasa tunajenga tenki la chini lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni mbili," alisema Mhandisi Njau.

Alisema utekelezaji wa mradi huo utahusisha ulazaji wa mabomba ya kusafirisha maji kutoka kwenye tenki kuanzia inchi 10 hadi inchi tatu.

"Kazi zinazofanyika ni pamoja na kulaza mabomba ya kusafirisha maji kutoka kwenye tenki ambapo itatekelezwa, kwa sasa tupo katika hatua ya manunuzi ya mabomba hayo," aliongeza.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Msongola, Venance Mwakilembe, alisema utekelezaji wa mradi wa maji Yangeyange ni neema kwa wakazi hasa wa mtaa wa Yangeyange kwa kuwa watanufaika na huduma ya majisafi na salama.

"Naipongeza DAWASA kwa kuanza utekelezaji wa mradi huu wa maji ambao utasaidia kutoa huduma ya maji kwa wakazi wa Yangeyange ambao wanapata shida ya maji kwa kipindi kirefu," alisema Mwakilembe

Mradi wa maji Yangeyange ambao chanzo chake cha maji ni kisima chenye uwezo wa kuzalisha maji lita 110,000 kwa saa kilichopo katika eneo la Mgeule pamoja na chanzo cha maji Mradi wa maji Nzasa - Somelo ni kisima chenye uwezo wa kuzalisha maji elfu 60,000 kwa saa.

Mradi huo unatarajiwa kukamilika Februari, mwakani ambapo utanufaisha wakazi wapatao 206,253.

# Bil. 5.14/- zanunua vifaa vya maabara shule 234 sekondari

SERIKALI katika mwaka wa fedha 2022/23, imetenga Sh. bilioni 5.14 kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara kwa shule 234 za sekondari za kata.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbozi (CCM), George Mwenisongole.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itapeleka vifaa vya maabara kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi katika shule za sekondari jimbo la Mbozi.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema serikali imekuwa ikipeleka fedha katika shule za sekondari kwa ajili ya umaliziaji wa miundombinu mbalimbali zikiwamo maabara za masomo ya sayansi.

Katika kufanya hivyo, alisema serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21 na 2021/22 imepeleka vifaa vya maabara katika shule za sekondari 1,258 nchini zilizokamilisha ujenzi wa vyumba vya maabara zikiwamo 12 katika wilaya ya Mbozi.

"Serikali itaendelea kugawa vifaa hivyo nchini ikiwa ni pamoja na shule za wilaya ya Mbozi kwa kuzingatia mahitaji na upatikanaji wa fedha na wadau mbalimbali," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alisema jimbo hilo lina shule 44 lakini zilizopelekewa vifaa ni 12 na kuhoji serikali inatoa kauli gani kupitia fedha hizo kupeleka vifaa kwenye shule ambazo hazina.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Silinde alisema serikali itapeleka fedha kwa ajili ya shule ambazo zitakuwa zimekamilisha ujenzi wa maabara kwa mwaka ujao wa fedha 2022/23 na zile ambazo zimenunuliwa vifaa taarifa zinasubiriwa ili vipelekwe.

Naye Mbunge wa Mbulu Vijijini (CCM), Flatei Massay, alihoji lini vitapelekwa vifaa vya maabara za sayansi kwa shule za sekondari 11 za jimbo hilo.

Silinde akijibu swali hilo, alisema kwenye shule zote ambazo zimekamilisha ujenzi wa maabara kwenye jimbo hilo vifaa hivyo vitapelekwa.






Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama (kulia), akijadiliana jambo na Mbunge wa Mbulu Mjini, Zacharia Isaay, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wizara yataja athari wenza kuishi tofauti

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imetaja athari nne za kijamii zinazotokana na watumishi wenza kuishi mbali na watoto wao ikiwamo kuvunjika kwa ndoa.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mwanaidi Ali Khamisi, alitaja athari hizo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Husna Sekiboko, aliyetaka kujua athari za kijamii kwa watumishi wenza kuishi mbali na watoto wao.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alikiri kuwapo na madhara ya kijamii kwa watumishi wenza kuishi mbali na watoto.

"Familia ni taasisi muhimu katika kuleta ustawi kwa jamii na taifa kwa ujumla. Ni kweli kuwa yako madhara ya kijamii kwa watumishi wenza kuishi mbali na watoto wao," alisema.

Alitaja athari hizo ni kuongezeka kwa vitendo vya ukatili kwa watoto majumbani, kukosa malezi chanya, hivyo kusababisha watoto kuathirika kisaikolojia, watoto kutokupata lishe bora hali inayochangia udumavu na mmomonyoko wa maadili na kuvunjika kwa ndoa kunakosababisha watoto wa mtaani.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zainab Katimba, alitaka kujua mkakati wa serikali wa kukabiliana na athari hizo.

"Nini kauli ya serikali kwa waajiri wale ambao hawatoi fursa ya kuhakikisha wafanyakazi wao wanapata haki ya kufanya kazi karibu na wenza wao?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri alisema serikali kupitia Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) imeunda kamati maalum za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake kwa ngazi zote.

Naibu Waziri aliwashauri wabunge kujifunza kukaa na watoto wao wakati wote ili kuwapa elimu mbalimbali za kijamii.

Akiongezea majibu ya swali hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alilihakikishia bunge kuwa ofisi hiyo ina dhamana ya kuangalia ustawi wa watumishi wa umma nchini kutokana na kutambua athari hizo.

Kutokana na suala hilo, alisema Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo ametoa waraka ambao unatoa fursa kwa mtumishi kuhamia kwa mwenza wake endapo eneo husika litakuwa na nafasi na atakuwa na uthibitisho wa vyeti vya ndoa na nyaraka zingine.

"Nitoe wito kwa waajiri wote kuzingatia waraka huu ili kusaidia ustawi wa familia, malezi ya watoto na kuhakikisha wafanyakazi wetu wanakuwa na fursa ya kuishi na wenza na kuzingatia miongozo iliyowekwa na menejimenti ya utumishi wa umma," alisema.

# Viwanja 4 vya ndege kujengwa kwa ufadhili

MIRADI ya ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora, Sumbawanga na Shinyanga, inatarajiwa kutekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), bunge lilielezwa jana mjini hapa.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alisema hayo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Christina Mnzava.

Dk. Mnzava alihoji lini serikali itaanza ujenzi wa uwanja wa ndege wa Shinyanga kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kasekenya alisema uwanja huo ni moja ya miradi ya ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege nchini.

Kasekenya alisema mpaka sasa, matakwa ya kimkataba kati ya serikali na EIB yamekamilishwa na mfadhili tayari ameshatoa fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo.

Aidha, alisema Mhandisi Mshauri pamoja na makandarasi wameonyesha utayari wa kuanza kazi na mikataba kati yao na serikali imeshatiwa saini tangu mwaka 2017.

"Kwa kuwa mradi huu umechelewa kuanza kwa wakati, mhandisi mshauri pamoja na makandarasi wameomba ongezeko la fedha katika kipengele cha 'price adjustment' ili kuendana na mabadiliko ya bei ya bidhaa na vifaa katika soko.

"Marekebisho haya yameshafanyika na kuwasilishwa kwa mfadhili kwa ajili ya kupata idhini ili 'addenda' zitiwe saini," alisema.

Pia alisema mkandarasi ameelekezwa kuwasilisha hati za dhamana za malipo ya awali ili malipo hayo yafanyika na kuanza utekelezaji wa mradi huu.

Alisema serikali imejipanga kuanza utekelezaji wa mradi huu kabla ya mwaka wa fedha 2021/22 haujaisha endapo mkandarasi atawasilisha hati ya dhamana ya malipo ya awali kwa wakati.

Akiuliza swali la nyongeza, Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, alisema mkoa wa Singida upo karibu na makao mkuu ya nchi Dodoma na kutokana na sababu za kiusalama uwanja wa Ndege Singida ni muhimu.

"Marais wote wawili, Hayati John Magufuli na Rais Samia Suluhu Hassan walisema katika viwanja 11, kiwanja cha Singida kitajengwa. Sasa naomba kujua lini serikali itatenga fedha kujenga uwanja ule ambao upo karibu na Makao Mkuu ya Nchi,"alisema.

Naibu Waziri Kasekenya akijibu swali, alikiri viongozi hao kuahidi uwanja huo kujengwa na kwamba Wizara ina mpango wa kufanya tathmini ya uwanja huo ili ujengwe.




Ukurasa 13

Tunapongeza anwani za makazi lakini, mh!

# BUFE

IJUMAA APRILI 15, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



**Bodi ya Utalii tunajinasibu ugeni wa watalii 900 kutua kwa mpigo**

Ukurasa 14

# Ana chipu katika ngozi, kidole chawa mbadala wa 'smart card'

**Na Mwandishi Wetu**

PATRICK Paumen (37) husababisha mshangao kila anapolipia kitu dukani au kwenye mgahawa. Hahitaji kutumia kadi ya benki au simu yake ya mkononi kulipa, badala yake anaweka tu mkono wa kushoto karibu na kasi inasoma.

Nuru ndogo ya mwanga iitwayo 'Led' chini ya ngozi yake kisha huangaza mara moja na malipo kufanyika, sasa Patrick anaeleza kwa kujidai "Mwitikio ninaoupata kutoka kwa washika fedha hauelezeki." Mkazi huyo wa Uholanzi, anasema anaweza kufanya malipo kwa kutumia mkono wake, kwa sababu mwaka 2019 aliwekewa kifaa kidogo cha malipo, yaani chipu yenye ukubwa kuzidi kiasi punje ya mchele, kilichoingizwa chini ya ngozi yake.

"Utaratibu huo unauma kama vile mtu anapoifinya ngozi," asema Paumen na hutoa mwanga wakati malipo yanafanywa.

Chipu aina hiyo ilipandikizwa kwa binadamu kwa mara ya kwanza mwaka 1998, teknolojia hiyo ilipokuwa inaanza kuchukua nafasi kibiashara na inapokuja suala la malipo kupitia chipu zinazoweza kupandikizwa, kampuni ya Uingereza - yenye makao yake huko Poland, Walletmor, inasema mwaka jana ilikuwa kampuni ya kwanza kuziuza.

Kipandikizi hicho kinaweza kutumika kufanya malipo katika nchi kama Marekani na Ufaransa, iwe migahawani, kunyolewa nywele au madukani.

Chipu ya Walletmor, ambayo uzito wake ni chini ya gramu moja ikiwa ndogo zaidi, inajumuisha antena.



Matumizi ya kidole mbadala wa 'smart card.' **PICHA: MTANDAO.**

Paprota anaongeza kuwa ni salama kabisa, ina kibali cha udhibiti, inafanya kazi mara tu baada ya kupandikizwa, na itakaa imara mahali pake, haihitaji betri au chanzo kingine cha nishati.

Kampuni iliyotengeneza inasema kwa sasa imeuza zaidi ya chipu 500 na teknolojia ambayo Walletmor hutumia, ni mawasiliano ya karibu kwenye mfumo wa malipo wa kielektroniki katika simu ya mkononi.

Mbali na hiyo, anasema na vipandikizi vingine vya malipo, ni vya utambulisho wa mitabendi za redio (radio-frequency identification au (RFID), teknolojia ambayo kwa kawaida hupatikana katika kadi za malipo za mkopo za kielektroniki.

Picha ya x-ray nazo huonyesha kipandikizi cha Walletmor, ambacho huingizwa kwenye mkono wa mtu baada ya kumfanya awe katika hali ya kupotewa na fahamu.

Kwa watu wengi wazo la kupandikizwa chipu kama hiyo mwilini, wanasema ni suala linguzi wa mwaka 2021 kwa zaidi ya watu 4,000 nchini Uingereza na Umoja wa Ulaya, uligundua asilimia 51 wangeweza kufanyiwa.

Hata hivyo, bila kutoa idadi ya asilimia, ripoti hiyo iliongeza kuwa 'uvamizi na masuala ya usalama umebaki kuwa kero kubwa' kwa waliohojiwa, lakini kwake Pauman anasema hana hofu yoyote katika hilo.

"Vipandikizi vya chipu vina aina ileile ya teknolojia ambayo watu hutumia kila siku," anasema na kuongeza: "Umbali wa kusoma hupunguzwa na koili ndogo ya antena ndani ya kipandikizi."

Kipandikizi huwa kinahitajika kuwa ndani ya sehemu ya sumaku umeme inayooana na RFID. Sasa ni wakati tu, ambao muunganisho wa sumaku kati ya msomaji na kifaa, ndio kipandikizi kinachoweza kusomwa na chipu za RFID hutumiwa zaidi kwa wanyama wa nyumbani kuwatambua wanapopotea.

"Haiwezekani kuwapata kwa kutumia kipandikizi cha chipu cha RFID - mnyama anayepotea anahitaji kupatikana kimwili," anasema mtalaamu na kuongeza:

"Bado suala la chipu kama hizo, (kinachosababisha wasiwasi) ni kama katika siku zijazo zitakuwa za hali ya juu zaidi, na kujazwa data binafsi ya mtu."

Mtaalamu Theodora Lau, na Mwandishi Mwenza wa Kitabu cha 'Beyond Good: How Technology Is Leading A Business Driven Revolution' anasema chipu za malipo zilizopandikizwa ni 'mwendelezo tu wa mtandao wa mambo, akimaanisha, ni njia nyingine mpya ya kuunganisha na kubadilishana data.

Theodora Lau, anafafanua kuwa ndani ya siku zijazo tutahitaji kujua mpaka wetu linapokuja suala la vipandikizi kama hivyo.

Hata hivyo, anasema kwamba watu wengi wako tayari kwa wazo hilo - kwani litafanya malipo kufanyika kwa haraka na rahisi - faida lazima ziwe za juu kuliko hatari, kwani chipu hizo zinapopachikwa mwilini zinabeba habari kibinafsi za mtu.

"Tuko tayari kulipa kiasi gani kwa ajili ya malipo kufanyika kwa urahisi?" anasema Theodora, akihoji undani: "Tunahitajika kuweka wapi mpaka linapokuja suala la faragha na usalama? Nani atakuwa akilinda miundombinu muhimu na wanadamu ambao ni sehemu yake?"

Paumen pia ana sumaku zilizopandikizwa kwenye vidole vyake. Huko kwao Uholanzi, chipu ya malipo ya Pauman ina taa ya LED iliyojengewa nyumbani inayoendeshwa na nguvu kutoka kwenye mwili wake.

Anajielezea mwilini mwake ana vipandikizi 32 kwa jumla, ikiwamo chipu ya kufungua milango. Anajigamba: "Teknolojia inaendelea kubadilika, kwa hivyo ninaendelea kukusanya zaidi... vipandikizi vyangu huongeza mwili wangu. Nisingependa kuishi bila hivyo."

**Kwa mujibu wa BBC**

BIASHARA

KUPAA BEI ZA BIDHAA...

# Waziri Dk. Kijaji aainisha vyote na darasa la usomi 'kwanini hivi'

- Ngano, mafuta kula, mbolea shida endelevu
- Vya nchini havijayumba, ole wao wapotoshaji

**Na Christina Mwakangale**

UMETIMU wastani wa mwezi mmoja mjadala uliotawala kwenye jamii nchini ni kupanda bei za bidhaa, zikiwamo vyakula, ambazo ndilo hitaji la kwanza na muhimu kwa binadamu.

Orodha hiyo inajumuisha sukari, ngano, mafuta ya kula , petroli na dizeli, zikiwa huduma muhimu kwa watu wengi na haziepukiki. Hatimaye serikali imetolea majibu chanzo cha bei hizo kubwa.

Katika kuelezea hilo ikiwamo sababu za kupanda bei kwa bidhaa hizo na nyingine, serikali imezitaja vyanzo vinne: Vita vinavyoendelea kati ya Russia na Ukraine; athari za Uviko-19, ongezeko la gharama za usafirishaji' na uhaba wa makasha (kontena) za kubebea mizigo.

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji amesema wiki hii kwamba katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita, serikali imekuwa ikifuatilia suala hilo na uchunguzi umebaini mambo kadhaa.

Waziri anaeleza, mgogoro kati ya Russia na Ukraine umeathiri mwenenedo wa bei ya baadhi ya bidhaa duniani ikiwamo Tanzania, huku kuwapo janga la Uviko -19 limesababisha uchumi kwenye maeneo mengi kufungwa, kama moja ya njia za kukabiliana na ugonjwa wenyewe, bidhaa na rasimali hazihami kutoka nchi moja kwenda nyingine.

Kadhalika, Dk. Kijaji anataja upungufu wa bidhaa katika soko la dunia kutokana na kusimama uzalishaji viwandani na kuongezeka gharama za usafirishaji kunako sababishwa na kukosekana makontena ya kubebea mizigo, eneo linalopelekea kupanda gharama usafirishaji mzigo mfano kutoka China, imepanda mara tano.

**RUSSIA VS UKRAINE**

Dk. Kijaji ambaye pia ana taaluma ya uchumi na soko la kimataifa, anasema bidhaa zenye mfungamano wa moja kwa moja na mgogoro kati ya Russia na Ukraine, zimeiathiri Tanzania kwa bei juu. Hapo anataja ngano, mafuta ya kula, mbolea, petroli, dizeli na mafuta ya taa.

Dk. Kijaji anaelezea nchi nyingi za Afrika huagiza ngano kwa wingi kutoka Russia na Ukraine kila mwaka ikikadiriwa kufikia dola za kimarekani bilioni nne sawa na Sh. trilioni 9.6.

"Mnufaika mkubwa katika uagizaji huu ni Misri ikifuatiwa na Sudan, Nigeria, Tanzania, Algeria, Kenya na Afrika ya Kusini," anasema, akitaja takwimu kimataifa, zinaonyesha mwaka jana Tanzania ilikuwa ya 53 kwa uagizaji ngano kwa wingi nje duniani, asilimia 57 ikitoka Ukraine na Russia ambako ndiko inanunuliwa kwa wingi.

"Kwa wastani Tanzania inaagiza na kuingiza nchini ngano tani 800,000, huku uwezo wetu wa kuzalisha ngano ndani ya nchi ikiwa ni wastani wa tani 100,000 kwa mwaka.

"Hivyo, tunaweza kuona ni kwa kiasi gani vita kati ya nchi mbili hizi ilivyo na athari za moja kwa moja kwenye bei ya ngano ndani ya taifa letu," anasema waziri.

Kwenye mafuta ya kula, Dk. Kijaji anasema nako kunaegemea athari za vita hivyo vya Russia na Ukraine, akisema mwaka 2019 kabla ya janga la Uviko-19 lilipaisha bei ya mafuta ya kula ilikuwa Dola za Marekani 700 (Sh. milioni 1.610) kwa tani moja ya mafuta, huku wakati wa janga la Uviko-19, bei yake ikiongezeka zaidi ya mara mbili kufikia Dola za Marekani 1,760 (Sh.milioni nne,) kwa tani moja ya mafuta ya kula mwaka 2020/21.

"Baada ya kuanza kwa vita ya Russia na Ukraine, dunia imeshuhudia bei ya mafuta ya kula ikipanda kutoka dola za kimarekani 1,760 kwa tani moja mwaka 2020/21 hadi kufikia dola 1,980 kwa tani moja mwaka 2022.

"Ongezeko hili la bei ya mafuta duniani lina athari hasi kubwa kwetu Watanzania, kwani uhitaji wa mafuta ndani ya taifa letu kwa mwaka ni tani 650,000 huku uwezo wetu wa kuzalisha mafuta ni tani 270,000 ambayo ni sawa na asilimia 41.5 tu ya mahitaji yetu kwa mwaka," anabainisha Dk. Kijaji.

Anasema, ongezeko lolote la bei ya mafuta ya kula kwenye soko la dunia lina athari hasi kwa bidhaa kwenye soko la ndani.

**MBOLEA**

Dk. Kijaji anaitaja mbolea ni bidhaa iliyoathirika sana na janga la Uviko-19, pia vita tajwa, akitoa takwimu mwaka 2019 kabla ya janga Uviko – 19, katika soko la dunia tani moja iliuzwa kwa Dola za Marekani 396 (Sh.950, 400), lakini baada ya Uviko mwaka jana ikapaa kuwa Dola 551 (Sh.1, 322,400).

Pia, anataja mbolea aina ya Urea iliuzwa Dola za Marekani 249 (Sh. 597, 600) hadi mwaka jana Dola 362 (Sh.868, 800).

"Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 vita kati ya Russia na Ukraine vikiendelea bei za mbolea hizo zimepanda hadi kufikia Dola 1,012 (DAP Sh. Milioni 2.428) na Dola 1,214 kwa Urea (Sh. milioni 2.9.

"Ongezeko hili la bei ya mbolea duniani lina athari hasi kubwa kwetu Watanzania, kwani uhitaji wa mbolea ndani ya Taifa letu kwa mwaka ni tani 700,000 ikilinganishwa na uwezo wetu wa kuzalisha mbolea tani 30,000 kwa mwaka.

"Maana yake ni kwamba, ongezeko lolote la bei ya mbolea kwenye soko la dunia lina athari hasi za moja kwa moja kwenye bei ya bidhaa hiyo kwenye soko letu la ndani.

"Ndiyo maana mwaka 2019 bei ya mfuko mmoja wa kilo 50 wa mbolea aina ya DAP uliuzwa kwa shilingi 57,886 na UREA uliuzwa kwa shilingi 52, 000," anasema Dk. Kijaji.

Anasema mwaka jana mfuko wa ujazo huo, uliuzwa kwa shilingi 66,995 (DAP) na shilingi 55,869 (Urea) na kupanda mara mbili mwaka huu baada ya kuanza kwa vita.

"Tumeshuhudia mfuko mmoja wa mbolea ya DAP ukiuzwa kwa shilingi 110,000 (DAP) na shilingi 104,000 (UREA). Hii ina maana kubwa sana kwani nchi za Russia na Ukraine ni wazalishaji na wasambazaji wakubwa wa bidhaa ya mbolea kwa gharama nafuu duniani ikilinganishwa na nchi nyingine.

"Tanzania imekuwa ikiagiza kiasi kikubwa cha mbolea kutoka katika nchi za Russia na Ukraine. Kwa mfano, katika msimu wa kilimo wa 2019/20 TFRA ilitoa vibali vya kuagiza jumla ya tani 17,376 za mbolea kutoka nchini Russia na tani 75,947 kutoka nchini Ukraine.

"Msimu wa kilimo wa 2020/21 TFRA ilitoa vibali vya kuagiza jumla ya tani 64,117 za mbolea kutoka nchini Russia," anaeleza, akifafanua katika msimu wa kilimo 2021/22 unaoisha sasa, TFRA ilikwishatoa vibali vya kuagiza tani 34,400 za mbolea aina ya NPK na UREA kutoka nchini Russia.

**PETROLI, DIZELI & TAA**

Kuhusu nishati mafuta, Dk. Kijaji anasema petroli, dizeli na mafuta ya taa, nazo zimeathirika. Anatoa mifano linganifu bei ya mafuta ya petroli katika soko la dunia ilikuwa Dola za Marekani 594.82 (Sh.milioni 1.4) kwa tani moja ya petroli kabla ya Uviko 19, lakini mwaka jana tani hizo ilifikia Dola 671.04 (Sh milioni 1.6).

Anasema kupaa bei kulichochewa zaidi na vita vya Russia na Ukraine na mwezi Januari hadi Machi mwaka huu, tani moja ya petroli iliuzwa Dola za Marekani 942.13 (Sh. milioni 2.27).

Waziri anasema bei katika soko la dunia mwaka 2019 kabla ya Uviko-19 ilikuwa Dola za Marekani 576.20 kwa tani, ikilinganishwa na kipindi cha Uviko-19 mwaka jana, bei ilishuka kidogo wastani wa dola 574.71 (Sh. million 1.38) kwa tani.

"Kipindi cha Januari hadi Machi, 2022 vita kati ya Russia na Ukraine vinaendelea bei ya bidhaa hiyo ilipanda maradufu hadi kufikia wastani wa Dola za Kimarekani 881.88 kwa tani moja. Bei ya mafuta ya taa katika soko la dunia mwaka 2019 kabla ya Uviko-19 ilikuwa ni wastani wa Dola za Marekani 594.94 (Sh. milioni 1.43) kwa tani moja ikilinganishwa na mwaka 2021 kipindi ikiuzwa dola 580.35 (Sh. milioni 1.39) kwa tani moja," anasema Dk. Kijaji.

"Kupanda kwa bei ya bidhaa hizi kuna athari ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja na bei za bidhaa na huduma nyingine. Mfano, unakuta mtu anauliza kwanini vita ya Russia na Ukraine inasababisha bei ya kokoto au mchanga kupanda.

"Jibu lake ni rahisi tu, mchanga au kokoto vinasafirishwa kwenye magari yanayotumia mafuta ambayo yamepanda bei," anafafanua mchumi huyo.

**MAELEKEZO SERIKALINI**

Dk. Kijaji anasema, serikali baada ya kubaini hilo, imeelekeza mamlaka zinazohusika kusimamia soko la bidhaa, zichukue hatua za kisheria kila penye chanzo cha kupanda bei, hasa panako thibitika upotoshaji wa wafanyabiashara.

"Baada ya taarifa yangu kwa umma, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kupitia kwa Katibu Mkuu, ilitoa ufafanuzi kwa umma kwamba Sheria ya Ushindani ndiyo mama inayotumika kudhibiti vitendo vya kuvuruga mwenendo we bei sokoni," anafafanua, akirejea Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2003.

**VIWANDA NA BIASHARA**

Dk. Kijaji anasema, tathmini iliyofanywa kufuatilia mwenendo wa mabadiliko ya bei za bidhaa katika soko nchini, inataja msingi ya kuzingatiwa kwenye mabadiliko ya bei.

"Mgogoro wa Russia na Ukraine, tathmini iliongeza jukumu hili. Nini matokeo ya tathmini ya mwenendo wa bei? Tathmini ya kina iliyofanyika imeonyesha kwamba bei ya bidhaa nyingi zinazozalishwa nchini zina uhimilivu mkubwa (stable),"anasema.




Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Dk. Ashatu Kijaji, akizungumza kuhusu sababu za kupanda bei bidhaa na hatua za serikali kukabili hali hiyo, kwenye mkutano na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **"Tanzania imekuwa ikiagiza kiasi kikubwa cha mbolea kutoka katika nchi za Russia na Ukraine. Kwa mfano, katika msimu wa kilimo wa 2019/20 TFRA ilitoa vibali vya kuagiza jumla ya tani 17,376 za mbolea kutoka nchini Russia na tani 75,947 kutoka nchini Ukraine.**



TAFAKURI YA MLALAHOI

## Tunapongeza anwani za makazi lakini, ila mh!






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

ZIPO nyakati mimi humtafakari na hatimaye kumkubali Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba, kwa kauli na maoni yake kuhusu maisha na mifumo ya maisha kwa ujumla wake, kwani hupenda kusema kwa mifano ya kujenga.

Juzi kati hapa nikamsikia akitoa mfano wa sisi na Wazungu, jinsi ambavyo Wazungu hujifanya kutuzidi akili na kurahisisha mambo kwa teknolojia na sayansi zao. Kishimba alizungumzia jinsi kuku wa kienyeji walivyobadilishwa na Wazungu na kuja na 'broila'.

Akaonyesha jinsi kuku hao wa kisasa wanavyokua na kukomaa baada ya miezi mitatu au sita na kutosha kuliwa, tofauti na wale wa kienyeji ambao huchukua muda mrefu sana. Pia, akatoa wa miti na hasa kutokana na mahitaji ya kuni na mkaa.

Akahoji kwanini kama Wazungu waliweza kuja na kuku wa kisasa wanaokua kwa muda mfupi na kutosha kuliwa, wasije na miti inayoweza kukua kwa miezi mitatu na kutosha kuchomwa mkaa au kukatwa kuni?

Ni mawazo ya kufikirisha sana, kwani hivi zasa tunawindana tukikata miti na kuchoma mkaa au kutumia kama kuni, kwa sababu tunaharibu mazingira, sasa ili kutafuta jinsi ya kuyalinda, tukipata miti inayokua haraka hivyo, litakuwa wazo jema.

Ameniathiri nami nikaona naweza pengine kuja na mawazo mbadala katika kazi hii inayoendelea ya kuandikisha anwani za makazi, ambayo imepamba moto kwelikweli nchi nzima, tukishuhudia viongozi wakihaha huku na kule, utadhani Uviko-22 imeingia.

Kila nikikaa na kufikiria hivi hii kazi ina ukubwa gani mpaka kuona viongozi wanazunguka huku na kule, kutoa elimu na mafunzo kwa watu wanaosimamia na kuitekeleza kazi hiyo ya kuandika tu majina ya mitaa na namba za nyumba.

Nikasikia mpaka kuna ndege zinaruka kwenda mikoani kupeleka viongozi kwa kazi hiyo! Inanifikirisha, kuwa hivi kila mwaka mmoja kabla ya uchaguzi mkuu tunapofanya uchaguzi wa serikali za mitaa tena kwa mabilioni ya pesa huwa ni wa nini?

Tunachagua viongozi wa mitaa mpaka vitongojini huko, tukiamini kuwa hawa ndio wanaomwakilisha Rais katika ngazi hizo za chini, ili kumtua mzigo wa kila kitu afanye yeye na hivyo hivyo kwa mawaziri, abaki anafanye yale ya kitaifa zaidi.

Sasa inapokuja kazi kama hii, mpaka waziri naye aende huko, si kupoteza fedha za umma kweli? Hivi kama ni suala la mtaa, bila yupo mjumbe wa nyumba 10 anayejua kila mkazi wake na ndiye awezaye kusimamia hilo na kukubaliana na wakazi wake.

Wakae pamoja na kama kuna wajumbe zaidi ya mmoja katika mtaa, wanakaa na kukubaliana mtaa wao uitwe jina gani, na nyumba iwe na namba gani, tayari ni anwani hiyo na matokeo ya makubaliano yanawasilishwa juu kwa Waziri kwa utekelezaji.

Mambo mengine ni watu kukaa na kujadili na kukubaliana na kupeleka mapendekezo juu, sawa tu na darasani wanafunzi wanakaa kikao chao chini ya kiranja na makubaliano yanapelekwa kwa mwalimu wa darasa, naye anasongesha juu, tatizo liko wapi?

Hii ni sawa tu na Mbio za Mwenge, eti ndio unakwenda kugundua udhaifu kwenye miradi kana kwamba unaona! Mwenge huo unasindikizwa na halaiki ya watu inayolipwa posho, mbali na posho ya mafuta ya Mwenge. Mwenge hauna macho ya kuona udhaifu, bali wakimbiza Mwenge!

Hivi huko iliko miradi, hakuna wakubwa wanaoweza kukagua na kuona udhaifu huo na kuchukua hatua kama si kupeleka maelezo ngazi za juu kwa ajili ya hatua? Tufike mahali jamani, tuhakiki uamuzi wetu tunaochukua kama una tija au ulaji tu!

Ni vizuri tukabadilika na wakati, hata kama kuna mambo yaliasisiwa na waasisi, lakini dunia inabadilika, twende nayo hivyo badala ya kubaki vilevile, dunia itatuacha tutalaumiana kwa kujifisidi wenyewe. Alamsiki!

BIASHARA

JAJI MIHAYO:

# Bodi ya Utalii tunajinasibu ugeni wa watalii 900 kutua kwa mpigo

- Mapato yaongezeka 76% kwa mwaka
- Mikoa Kusini nayo 'kuchele' kwa vivutio



Sehemu ya vivutio vinavyowagusa sana watalii nchini. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Beatrice Philemon**

UTALII hivi sasa iko katika orodha ya vinavyoshikilia uchumi kitaifa kukiwapo vivutio vingi vya utalii, lakini bado havijulikani kwa watalii wa ndani.

Baada ya kuona umuhimu huo wa kisekta kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) kwa kushirikiana na wadau wake kisekta, wakiwemo wakala wa utalii wa ndani na nje ya nchi, wametangaza vivutio vya utalii katika nchi mbalimbali duniani.

Katika masoko ya kimkakati yanayojumuisha nchi ya Israel ambapo mwezi huu Tanzania inatarajia kupokea watalii 961 kutoka Israel, kujionea vivutio vya utalii vilivyopo hapa nchini. Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Jaji Thomas Mihayo anaiambia Nipashe, jumla ya watalii 361 wamewasili Tanzania tarehe 9 mwezi huu na watalii 600 watawasili nchini Jumapili ijayo.

Ujio wa watalii kutoka nchi ya Israel nchini Tanzania, utasaidia vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania kujulikana nchini humo kusaidia Tanzania kupata fedha za kigeni, pia kuvutia watalii wengine kutoka Israel kutembelea Tanzania.

"Wakiwa nchini watapata muda wa kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii na hatimaye kuvitangaza katika nchi yao," anasema.

Jaji Mstaafu Mihayo anasema idadi ya watalii kutoka Israel, imekuwa ikiongezeka kila siku, licha ya ongezeko kuathiriwa na UVIKO-19.

Anasema mwaka 2015, jumla ya watalii 14,754 kutoka Israel walitembelea Tanzania kuona vivutio mbalimbali vya utalii.

Pia, mwaka 2016 watalii 22,967; hali kadhalika mwaka 2017 watalii 36,640; mwaka 2018 watalii 31,419; mwaka 2019 ilipokea watalii 16,348; mwaka 2020, Tanzania ilipokea watalii 6,889 na mwaka 2021 jumla ya watalii 6,303 walitembelea.

"Namshukuru Rais Samia Suluhu kwa kuunga mkono jitihada zetu mahsusi za kuitangaza Tanzania kimataifa kupitia programu maalum ya 'Royal Tour," anasema

Ni programu yenye mtandao maarufu wa habari nchini Marekani unaoitwa 'theGrio' unaorejea juhudi za Rais wa Tanzania kuiongoza vyema sekta ya utalii nchini na kuifanya Tanzania kivutio cha kwanza cha utalii Afrika mwaka 2022.

"Programu hii kwa ujumla imeanza kuleta matunda kwa kuvutia watalii na wawekezaji mbalimbali kuja nchini, mathalani wakala wa utalii zaidi ya 30 kutoka nchi masoko ya utalii zikiwemo Marekani, Ufaransa, Uingereza na Israel, waliohamasika kutembelea Tanzania kujifunza na kuona vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuvitangaza katika nchi zao," anaeleza.

Vilevile, wawekezaji wa Bulgaria nao wanatarajia kuwekeza katika huduma za malazi kimataifa, kwa kujenga pango la kitalii lenye hadhi ya nyota tano, zitakazoendeshwa na kampuni zenye hoteli kubwa katika Hifadhi za Taifa za Serengeti, Manyara, Tarangire na Ngorongoro.

**MAPATO YAONGEZEKA**

Sekta Utalii ndiyo inachangia wastani asilimia 17.5 ya pato la taifa na asilimia 25 ya fedha zote za kigeni, huku Jaji Mstaafu Mihayo akisema idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kwa asilimia 48.6; kutoka watalii 620,867 mwaka 2020 hadi 922,692 mwaka jana.

Anasema mapato yatokanayo na watalii kimataifa yanakadiriwa kuongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 714.59 (Sh.) mwaka 2020 hadi Dola za Marekani milioni 1,254.4 (Sh.) mwaka 2021 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 76.

Watalii wa ndani, pia wameongezeka kutoka watalii 562,549 mwaka 2020 hadi kufikia watalii 788,933 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 40.2.

Katika mapato yatokanayo na utalii wa ndani katika maeneo ya vivutio vya utalii, yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 9.7 mwaka 2020 hadi kufikia bilioni 12.4 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 27.8.

Kimsingi, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), imekasimiwa na serikali jukumu muhimu la kutangaza vivutio vya utalii nchini, kuhamasisha watalii wa ndani na nje kutembelea vivutio kwa lengo la kuiingizia taifa mapato ya kigeni.

Vilevile, wawekezaji kutoka Taifa la Bulgaria wanakusudia kuwekeza huduma za malazi yenye hadhi kimataifa ya nyota tano katika Hifadhi za Taifa za Serengeti, Manyara, Tarangire na Ngorongoro, zikiendeshwa na kampuni maarufu.

Anasema ni hatua itakayoleta matokeo chanya katika kuongeza idadi ya vyumba na wigo wa mnyororo wa huduma katika sekta ya utalii.

**MKURUGENZI TTB**

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Utalii Tanzania, Felix John, anasema kuwa ujio wa watalii hao wa Israel na nchi nyinginezo, ni zao la mikakati waliyoifanya TTB, akifafanua:.

"Tumefanya ziara za mafunzo ikiwemo nchi ya Israel kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania, kushiriki maonyesho ya kimataifa ya utalii katika nchi mbalimbali na kutumia 'goodwill ambassadors' (mabalozi wenye nia njema) ambao wapo katika nchi ya Marekani, Uingereza, China, Russia, Italia," anasema

Mwaka jana, madaktari kutoka Israel walifika Tanzania kuangalia hali ya Uvico -19 na usalama wa watalii wao, hata wakaridhika na hali ilivyo hata wakawavutia watalii wa Israel kutembelea nchini.

John anasema, serikali kwa sasa imeanza kuboresha miundombinu kuvutia watalii wengi kutembelea ukanda wa Kusini, huko nao TTB ikitarajia kupokea watalii wengi zaidi wa ndani na nje kutembelea maeneo hayo.

Anaainisha miundombinu hiyo ni kama vile barabara nzuri, hoteli na mawasiliano, ili mtalii mhitaji atembelea vivutio akivifikia kirahisi nchini.

"Kinachochangia idadi kubwa ya watalii kwenda kutembelea ukanda wa Kaskazini ni ubora wa miundombinu, viwanja vya ndege vilivyopo katika maeneo hayo, pia kubarikiwa kwa kuwa na vivutio vya kipekee ambavyo ni maarufu duniani, mfano Mlima Kilimanjaro ambao ni mkubwa katika Bara la Afrika, Ngorongoro Crater," anasema

Sekta hii pia inachangia takriban asilimia 17.5 ya Pato la Taifa na wastani wa asilimia 25 ya fedha zote za kigeni.




Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii, Jaji Mstaafu Thomas Mihayo.

# Rais Samia mgeni rasmi Mei Mosi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) yatakayofanyika kitaifa Jijini Dodoma.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu mkoa wake kuwa mwenyeji wa maadhimisho hayo.

Alisema mkoa wa Dodoma umepewa heshima ya kuwa mwenyeji wa sherehe za Mei Mosi kitaifa ambayo alisema yatakuwa tofauti na ya miaka iliyopita.

Mtaka alisema wiki ya maandalizi ya Mei Mosi mwaka huu itaanza rasmi kesho hadi Aprili 30, mwaka huu, na kilele kitakuwa Mei Mosi.

"Katika kufikia azma ya serikali ya kuhakikisha kila fursa inayojitokeza inachangia ujenzi wa uchumi imara, uongozi wa mkoa wa Dodoma kwa kushirikiana na wadau, umeazimia kutumia fursa ya Mei Mosi kitaifa kuziunganisha sekta zote za kiuchumi kwa manufaa mapana.

"Aidha imepanga pia kuandaa maadhimisho ya kipekee kwani ni maadhimisho ya pili kwa Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

Mtaka alisema kuanzia kesho hadi Aprili 30, kutakuwa na maonyesho ya michezo mbalimbali ikiwamo soka, netiboli, kuvuta kamba, kufukuza kuku, drafti, bao na riadha ambayo itafanyikia katika Uwanja wa Jamhuri, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohanam Kilimani Viterani, Sheli Wajenzi, Chinangali Park, Vijana na Mtekelezo.

Katika hatua nyingine, alisema Aprili 20 hadi 30 kutakuwapo na maonyesho ya OSHA ambayo yatashirikisha makundi ya wajasiriamali wadogo na wa kati, taasisi za umma na za huduma, wafanyabiashara wa kati na wakubwa, taasisi za fedha, viwanda, vyama vya wafanyakazi, wizara na wadau wengine.

Pamoja na hayo, alisema kutakuwapo na huduma za upimaji wa virusi vya Ukimwi (VVU), uchangiaji wa damu na chanjo ya UVIKO-19. Aidha, alisema katika maadhimisho hayo kutakuwapo na midahalo mbalimbali kupitia vyombo vya habari ambayo itahusisha vyama vya wafanyakazi, waajiri na serikali sambamba na kutunuku wafanyakazi hodari ngazi ya mkoa pia kufanya ziara za utalii wa miradi.

Mtaka aliwataka wakazi wa jiji la Dodoma pamoja na wilaya jirani kutumia fursa kufanya biashara ili kujiingizia kipato huku akiwaonya wafanyabiashara wa nyumba za kulala wageni kutokuwa na tamaa ya kupandisha bei za vyumba.



Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, Kenath Yindi, akikagua masomo ya wanafunzi wa darasa la pili katika shule ya msingi Mizengo Pinda, kijiji cha Chinangali, alipoitembelea jana kwa ajili ya kukagua majengo ya madarasa mapya yaliyojengwa kwa fedha ya UVIKO-19. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Chamwino yapiga marufuku ufugaji holela

**Na Peter Mkwavila, CHAMWINO**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, imepiga marufuku ufugaji holela kwenye maeneo ya mijini na yasiyo rasmi.

Marufuku hiyo imetolewa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Kenneth Yindi, kutokana na malalamiko yaliyotolewa na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kuharibiwa na mifugo, miti yao iliyopandwa.

Yindi alisema hayo alipokuwa akizungumza na walimu na wanafunzi kwenye ziara ya kukagua maendeleo ya shule katika kata ya Buigiri. Alisema wafugaji wanatakiwa kuacha tabia ya kuchunga mifugo kwenye maeneo ya mijini na yasiyo rasmi kwa kuwa mifugo hiyo imekuwa ikiharibu mazingira.

Alisema serikali imetoa miti hiyo kwa ajili ya kupanda na kutunza katika maeneo ya majengo ya shule na taasisi mbalimbali zikiwamo za watu binafsi na serikali, hivyo ufugaji holela kwenye maeneo hayo haukubaliki.

"Moja ya changamoto kubwa niliyoelezwa kwenye ziara yangu hii ambayo nimeambatana na kamati yangu hii ya kata na kijiji ya maendeleo ya elimu ni baadhi ya wakazi walio karibu na maeneo ya shule mifugo yao kusababisha uharibifu wa miti iliyopandwa," alisema. Pia aliwataka wazazi na walezi kushirikiana na walimu ili kujua maendeleo ya watoto kitaaluma badala ya kuona jambo hilo ni la serikali peke yake.

Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi na awali ya Maki Brilliant, Shaibu Beya, akizungumza mbele ya kamati hiyo ya maendeleo ya elimu ya Kata na Kijiji, alisema kwenye eneo hilo la shule jumla ya miti 250 ilipandwa kati ya hiyo 30 imeharibiwa na mifugo.

Alisema changamoto iliyopo kwenye shule ni ufugaji holela wa mifugo kutoka kwa wananchi walio karibu na maeneo hayo hali ambayo imekuwa ikisababisha uharibifu wa mazingira.

Mwanafunzi Athony Mathias (10), anayesoma darasa la pili katika Shule ya Msingi ya Mizengo Pinda, alisema pamoja na serikali kutoa miti katika taasisi na shule bado kuna ulazima wa kuwaelimisha wafugaji ili kuepukana na uharibifu wa mazingira.

Alisema kuwa juhudi hizo za upandaji miti zimekuwa zikikwamishwa na wenye mifugo kutokana na tabia yao ya kuchunga katika maeneo yaliyopandwa bila kujali jitihada zilizotumika.

# Zahanati, hospitali binafsi zapewa onyo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MGANGA Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, amevitaka vituo vya afya, zahanati za sekta binafsi na zinazomilikiwa na taasisi za dini nchini kuacha kuikimbia serikali inapokwenda kufanya ukaguzi katika maeneno yao.

Akizungumza wakati akifungua mkutano uliohudhuriwa na zaidi ya washiriki 70 ambao ni wataalam wa huduma za afya kutoka sekta binafsi na taasisi za dini, Dk. Sichalwe alisema ukaguzi huo hauna nia mbaya bali unalenga kuhakikisha huduma bora za afya zinatolewa kwa wananchi.

"Ninawasihi mkubali kukaguliwa na halmashauri na mikoa husika maana hapa lengo ni kujiridhisha na ubora na usalama wa huduma mnazozitoa kwa wananchi na si vinginevyo," alisema Dk. Sichalwe.

"Kiu ya serikali ni kuona huduma za afya zinaboreshwa, hivyo sekta binafsi inatakiwa ijikite katika kutoa huduma bora kwani imebeba usalama wa raia, huduma bora za afya, hivyo ni muhimu ziwapo kwenye zahanati na vituo vyao vya afya. Mnapaswa mboreshe eneo la miundombinu, upatikanaji wa dawa na kuwapo na upatikanaji wa vifaa tiba vyenye ubora," aliongeza.

Pia aliwataka wamiliki wa huduma hizo kuboresha nidhamu ya watumishi wao na kuwe na muundo wa kiuongozi unaoeleweka na vituo vya kutolea huduma viwe vya kisasa. Sambamba na hilo, aliwataka kulenga kwenye kutoa huduma badala ya kufanya biashara.

"Sisi kama serikali tumepanua wigo wa kutatua changamoto za afya kwa kukaribisha sekta binafsi na mashirika ya dini kutoa huduma za afya kwa wananchi ili kusogeza huduma karibu nao," alisema.

Dk. Sichalwe aliomba ofisi yake ishirikishwe mapema katika mkutano kama huo utakaofanyika mwakani ili ishiriki na kuona changamoto kwa lengo la kuzitatua kwa pamoja.

Awali, Mkurugenzi wa Tume ya Kikristo ya Huduma za Jamii (CSSC), Dk. Josephine Ballati, alisema ubora wa huduma ni suala muhimu kwa sekta binafsi kuzingatia namna bora ambayo wanaweza kuboresha huduma ili wananchi wapate huduma bora za afya.

Alisema mkutano huo umehudhuriwa na wawakilishi kutoka zaidi ya vituo 70 lengo kubwa likiwa ni kufanya tathmini juu ya huduma wanazozitoa kwa wateja.



## Mradi wa maji kuwakomboa zaidi ya wananchi 20,000

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imetenga Sh. milioni 631 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mradi mkubwa wa maji ambao utajengwa katika Kata ya Itamboleo utakaohudumia wakazi zaidi ya 20,000 wa eneo hilo na maeneo jirani.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara uliowahusisha wananchi wa Itamboleo na Mkandarasi ambaye aliingia mkataba wa utekelezaji wa mradi huo.

Alisema fedha hizo zimetokana na mkopo wa masharti nafuu kwa ajili ya mapambano dhidi ya mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 ili kutatua tatizo la maji kwenye Kata ya Itamboleo.

"Rais wetu mpendwa Samia Suluhu Hassan, ametuletea fedha milioni 631 kwa ajili ya kukamilisha mradi wa maji unaojengwa katika Kata ya Itamboleo, zitapatikana fursa mbalimbali ikawamo ajira kwa wanakijiji," alisema Mfune.

Meneja wa maji Wilaya ya Mbarali (RUWASA), Mhandisi Samwel Hechei, alisema mradi huo unatekelezwa kwa awamu mbili, wa kwanza utakuwa ni wa banio, tangi la lita laki tatu, vituo vya kuchotea maji nane na ujenzi wa mtandao wa bomba kilomita 15.9.

Alifafanua kuwa awamu ya pili utatekelezwa katika vijiji vya Matebete, Mbalino na Kapunga na utahusisha ujenzi wa mtandao wa bomba lilomita 72.2, tangi la lita 200,000 pamoja na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 19. Na utagharimu Sh. milioni 3.9.

Akizungumzia mradi huo, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mbarali, Hashimu Mwalyawa alimpongeza Mkuu wa wilaya kwa kutekeleza vizuri Ilani ya CCM, amepongeza pia kwa kuleta mradi wa maji kata ya Itamboleo kwa kuwa walikuwa na shida ya maji.

Aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano wa hali na mali katika kutekeleza ujenzi wa mradi huo na kuwasihi kuepukana na vitendo vya wizi wa vifaa hivyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Itamboleo, Twalibu Lubandamo, alisema eneo hilo lilikuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji na kwamba mradi huo utasaidia kumtua mama ndoo kichwani.

Alisema mkataba wa utekelezaji wa mradi ulisainiwa Januari 10 mwaka huu na unatarajiwa kutekelezwa ndani ya miezi sita na kwamba ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi 22,543.

# Anwani za makazi kutofanyika eneo la hifadhi

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, amesema zoezi la anwani za makazi kwa sasa halitafanyika kwenye maeneo yote yanayodaiwa kuwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kupitia tangazo la serikali namba 28, hadi hapo serikali itakapotoa ripoti ya maeneo hayo kuthibitika kuwa ndani ya hifadhi au la.

Mfune alitoa kauli hiyo jana, wakati wa kikao cha tathmini ya zoezi hilo la anuani za makazi kilichowahusisha watendaji wa kata, vijiji na madiwani, ambalo linaendelea kufanyika wilayani Mbarali na kuhitimishwa Aprili 30, mwaka huu. Alisema hadi sasa baadhi ya maeneo yaliyoko Igava, Kilambo, Mwatenga, Miyombweni, Madibira na Kata yote ya Madibira, hayatafikiwa na zoezi hilo kwa sababu yako kwenye tangazo la serikali namba 28 yaani (GN28) ambayo inayatambua maeneo hayo kuwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Hata hivyo, akiwa katika mkutano wa hadhara katika Kijiji cha Mkunywa kilichopo Madibira, Mkuu wa Wilaya, Reuben Mfune alisema mawaziri wanane wametumwa kuzunguka maeneo yote yanayodaiwa kuwa katika hifadhi za taifa ili kufanya hitimisho.

Alisema wanaendelea kuchunguza na kufuatilia na baada ya kukamilisha watatoa taarifa kamili ya mgogoro huo baina ya vijiji na hifadhi.

Kutokana na hali hiyo aliwakumbusha wananchi kuacha kufanya shughuli zozote za kilimo, ufugaji na uvuvi kwenye maeneo yaliyo ndani ya hifadhi.

Mwenyekiti wa zoezi la anwani za makazi wilayani Mbarali, Geofrey Mwaijobele, alisema hadi sasa zoezi hilo limefikia asilimia 91 na linatarajiwa kukamilika Aprili 30, mwaka huu. Akizungumzia zoezi hilo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ubaruku, Ponsiano Mhavila, alisema wanaendelea kuwahamasisha wananchi kuchangia gharama za utengenezaji wa vibao ambavyo vinaendelea kuwekwa wenye mitaa na vitongoji na makazi ya watu.



Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, Ruben Mfune, akimtwisha ndoo ya maji, Mkazi wa kijiji cha Mwakaganga, Josephine Mtweve, alipotembelea kukagua maendeleo ya mradi wa maji wa Mwakaganga, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Bil. 1.9/- kukamilisha ujenzi daraja Mto Lyandembela

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

BAADA ya kilio cha muda mrefu kwa wananchi wa Kata ya Madibira wilayani Mbarali, Mkoa wa Mbeya, kuhitaji daraja la kudumu katika mto Lyandembela ili waweze kufanya shughuli zao ikiwamo kusafirisha mazao na bidhaa nyingine, serikali imepanga kutumia Sh. bilioni 1.9 kukamilisha ujenzi wake.

Kwa mujibu wa mwakilishi wa Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania, Mhandisi Frank Kamala, hadi sasa ujenzi wa daraja hilo umefikia asilimia 65.

Alisema ujenzi ulianza Julai 10, 2020 na unatarajiwa kukamilika Julai 28, mwaka huu na kutoa ajira nyingi kwa wakazi wa Kata ya Madibira.

"Kila mara tulikuwa tunafanya marekebisho ya daraja katika Mto Lyandembela kwa sababu linatumika kwenye shughuli mbalimbali ikiwamo kusafirisha mpunga na mazao mengine mashambani, kwa kuwa tulikuwa tunatumia gharama kubwa kufanya marekebisho hayo tulikubaliana kuanza ujenzi wa daraja jipya na kubwa ili kutojirudia tena kwa kikwazo hicho," alisema Mhandisi Kamala.

Alisema kukamilika kwa ujenzi wa daraja hilo kutasaidia wakulima pamoja na wafanyabiashara kusafirisha bidhaa zao bila usumbufu, pia wananchi wengine kusafiri bila vikwazo ikilinganishwa na ilivyokuwa awali.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Madibira, Imani Mbogela, alisema nyakati za mvua za masika walikuwa wanalazimika kuwavusha watoto katika mto wakihofia kusombwa na maji ambayo yalijaa hadi juu ya daraja Mto Lyandembela.

Alisema mara kadhaa walipaza sauti zao kuiomba serikali kuwajengea daraja lingine ambalo litakuwa imara ili kuendelea kufanya shughuli zao za uzalishaji mali kama kawaida.

"Daraja la Mto Lyandembela linaunganisha maeneo mengi ya kibiashara kutoka Wilaya ya Mafinga mkoani Iringa hadi mjini Mbarali hivyo kukamilisha kwa daraja linaloendelea kujengwa ambalo ni la kisasa na kubwa litachangia shughuli za kiuchumi na kuufanya mji wa Madibira kuendelea kukua kwa kasi kwa sababu ni eneo ambalo linatumika zaidi kwa kilimo cha mpunga, alizeti na mazao mengine ya biashara," alisema Mbongela.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Mkunywa, Kata ya Madibira akiwamo Monica Steward, alimshukuru, Rais Samia Suluhu Hassan kutenga kiasi hicho cha fedha ili kujenga daraja kubwa na la kisasa ambalo litatumika kwa miaka mingi.

Alisema kukamilika kwake kutafungua fursa mbalimbali za kiuchumi kutoka mikoa ya Mbeya na Iringa kwa kuwa biashara na shughuli nyingine za kilimo zitafanyika.







Baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Kusini Pemba, wakishiriki futari maalum iliyoandaliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi, mkoani humo juzi. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi ataka hatua wanaochelewesha uchumi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ili kujenga uchumi wa Zanzibar lazima hatua zichukuliwe dhidi ya mambo yanayorejesha nyuma ukuaji wake ikiwamo wizi na ubadhirifu wa mali ya umma.

Rais Mwinyi aliyasema hayo katika mkutano wake na wazee wa Baraza la Wazee wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Pemba, Tibirinzi, Chake Chake.

Alisema ni kawaida hatua hiyo ikichukuliwa wapo watu ambao hawatokuwa tayari kuipokea hali hiyo na kusema kwamba dhamira yake ni kuendelea kutekeleza ahadi zilizoahidiwa wakati wa kampeni.

Alisema kila eneo la miundombinu ya maendeleo ilitolewa ahadi wakati wa kampeni na kusisitiza haja ya kuchukuliwa hatua kwa wale wachache walio na dhamira potofu ya kutofikia malengo yaliyokusudiwa

Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa mara zote mabadiliko yanakuwa ni magumu kupokelewa, lakini ni vyema ikajulikana kwamba chochote kinachohusu serikali ni cha wengi na si cha mtu mmoja na suala la kupambana na ubadhirifu ni la lazima.

Alisisitiza kwamba licha ya ugumu wa kiuchumi, bado Serikali ya Zanzibar imo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo ya maji, umeme, barabara na miundombinu ya afya na elimu.

Alisisitiza kwamba lengo lake ni kuhakikisha anatimiza ahadi alizoahidi kwa wananchi na ndiyo maana amekuwa akichukua hatua kwa wale wabadhirifu na wasioendana na kasi yake ya utendaji wa kazi kwa dhamira njema ya kufikia ahadi zilizotolewa.

Alieleza umuhimu wa kuhakikisha Baraza la Wazee linafanya kazi zake ipasavyo kutokana na busara zao huku akiahidi kuendelea kushirikiana nalo kutokana na umuhimu wake.

Vile vile, alieleza hatua zinazochukuliwa na serikali kuhakikisha inapambana na mfumko wa bei ya bidhaa kutokana na changamoto za uchumi duniani ikiwa ni pamoja na kuondoa ushuru katika bidhaa mbali mbali ili kuzifanya bei zihimilike licha ya uwezo wa serikali kuwa na kikomo.

"Yapo mambo ambayo yako ndani na uwezo wetu na yapo ambayo yako nje ya uwezo wetu na kama hili liko nje ya uwezo wetu lakini tutajitahidi," alisema.

Kwa upande wao wajumbe wa Baraza la Wazee wa CCM Pemba, walimpongeza Dk. Mwinyi kwa juhudi zake anazozichukua tangu aingie madarakani huku wakiahidi kuendelea kumuunga mkono kwa kutambua juhudi zake za kuiletea maendeleo Zanzibar.

Katika taarifa yao iliyosomwa na Katibu wa Baraza hilo, Abdalla Yussuf Ali, ilieleza kuwa Baraza hilo lina kazi ya kutekeleza sera za chama na malengo ya serikali kwa wazee wenzao.

Dk. Mwinyi pia aliungana na wananchi wa Mkoa wa Kusini katika futari maalum aliyowaandalia.

# Serikali yaweka mikakati kukamilisha kesi za jinai

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imeweka mikakati kuhakikisha kesi za jinai zinakamilishwa uchunguzi wake kwa wakati na kutajwa mahakamani ili wahusika wapate haki kwa mujibu wa sheria.

Hayo yalisema na Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar Awadhi Juma Haji, wakati wa ziara yake katika taasisi mbalimbali ikiwamo zenye uhusiano na mwenendo wa makosa ya jinai kwa ajili ya kuleta ufanisi wa kazi na kusimamia kesi za jinai.

Kamishna huyo alisema, taasisi zinazofanya kazi na kushughulikia mwenendo wa sheria na makosa ya jinai zinahitaji kufanya kazi kwa pamoja na kuyafikia malengo ili jamii ipate haki zake kwa mujibu wa sheria.

Alisema yapo malalamiko yanaelekezwa kwa Jeshi la Polisi kuhusu kuchelewa kwa kesi kusikilizwa mahakamani ambayo wakati mwingine yapo kwa upande wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Alieleza kuwa wakati umefika sasa kuona ushirikiano wa taasisi hizo mbili unaimarishwa na zimepewa majukumu ya kufanya uchunguzi na kusimamia mwenendo wa makosa ya jinai.

"Tunatakiwa tufanye kazi kwa kushirikiana kwa sababu taasisi zetu hizi zimepewa majukumu makubwa ya kuona zitatekeleza majukumu ya haki za binadamu na sheria," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Mashtaka na Makosa ya Jinai, Salma Hassan, alisema ushirikiano unahitajika katika utekelezaji wa kusimamia haki za jinai ambazo misingi yake mikubwa ni utawala bora na haki za binadamu.

Alisema Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, imejipanga ikiwamo kuhakikisha kesi za jinai zinakamilishwa uchunguzi wake na kufikishwa mahakamani kwa ajili ya kusikilizwa.

Alisema wakati umefika kwa Jeshi la Polisi idara ya upelelezi kuhakikisha uchunguzi wa kesi unafanyika kwa wakati ili zifikishwe mahakamani na kutajwa.

"Kazi yetu kubwa kukamilisha uchunguzi wa kesi ambazo awali msingi wake umefanywa na Jeshi la Polisi na sisi kuzipitia upelelezi wake kabla ya kuzipeleka mahakamani na kutajwa," alisema. Kwa upande wake Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi (DCI) Zubeir Chembela, alisema miongoni mwa kazi kubwa inayofanywa na idara ya upelelezi ni kuwapatia mafunzo watendaji wa Jeshi la Polisi kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao vizuri kwa ajili ya kujiongeza kukabiliana na matukio ya uhalifu.

Alisema wahalifu wengi hivi sasa wamekuwa na mbinu mpya za kutenda uovu wao na mikakati mipya inahitajika ili kukamatwa na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

# Mkoa Kusini wapongezwa anwani za makazi

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, ameupongeza uongozi wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa kufanya vizuri katika zoezi la uwekaji wa anwani za makazi linaloendelea katika mkoa huo.

Dk. Khalid aliyasema hayo wakati wa ziara maalum ya kukagua na kuangalia zoezi hilo linavyotekelezwa na watendaji waliopewa kazi hiyo katika Shehia ya Jumbi mkoani humo.

Alisema kuwa, Mkoa wa Kusini Unguja umepiga hatua nzuri katika zoezi la uwekaji wa anwani za makazi (Post Code) katika Shehia na Mitaa na hadi sasa umefikia asilimia 76.

Alisema Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, itaendelea kufuatilia utekelezaji wake katika mikoa mingine kwa lengo la kuhakikisha unakamilika ndani ya wakati uliopangwa ili kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan na Dk. Mwinyi, mwezi Mei mwaka huu.

"Zoezi hili linatakiwa likamilike ndani ya mwezi Mei, hivyo sote kwa pamoja tunapaswa kufanya kazi kwa pamoja ili kufikia lengo lililokusudiwa," alisema Dk. Khalid

Akizungumzia fursa zikazo patikana baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, Dk. Khalid alisema litasaidia kurahisisha shughuli za kijamii ikiwamo kufungua fursa kwa wafanyabiashara.

Pia, mifumo maalum itasaidia kuiweka Zanzibar na Tanzania katika ramani ya dunia na kufungua milango kwa shughuli zitakazokuwa na maslahi kwa jamii.

"Kukamilika kwa zoezi hili kutaiweka Zanzibar katika ramani ya dunia, pamoja na kufungua milango ya fursa mbalimbali jambo ambalo nchi nyingi ulimwenguni zimeanza kwa muda mrefu" alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, alisema zoezi la uwekaji wa anwani za makazi katika mkoa huo linakwenda vizuri kutokana na mipango na mikakati imara waliyojiwekea.

Hadid alisema, Mkoa wa Kusini unatarajia kulikamilisha zoezi hilo ndani ya kipindi cha wiki moja na kutoa wito kwa wananchi wanaomiliki majengo kuviacha vitambulisho nyumbani ili kuwarahisishia watendaji wanaofanya kazi hiyo kufanya usajili bili ya usumbufu.

Vile vile, alisema zoezi hilo lina faida nyingi litakapokamilika na mwananchi hatopata usumbufu wa kuuliza wakati anapotaka kwenda sehemu baadala yake atatumia anwani hizo kumuelekeza.

Kwa upande wake Sheha wa Shehia ya Jumbi, Muhidini Haji Machano, alisema wananchi wanaoishi katika shehia hiyo wamelipokea vizuri zoezi hilo na ameshauri elimu zaidi itolewe ili kujenga uwelewa kwa wananchi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MULEBA MKOA WA KAGERA**

**MAOMBI MADOGO NA. 15/2022**

**ZEBADIA ZAKAYO……………………MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**1.EDIPHONCE RUSENENE 2. ALISTIDES ANDREA3.SIMON SIMON 4. VERIUS KILIMUGISHA……………….WAJIBU MAOMBI**

**KWA:1. ALISTIDES ANDREA 2. SIMON SIMON 3. VERIUS KILIMUGISHA**

**(POPOTE PALE ULIPO)**

Mnaarifiwa kuwa Maombi Na.15/2022 yamepangwa kutajwa tarehe 22.04.2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza,J.K.Banturaki saa2.30 asubuhi,mahali-Muleba(Mamlaka ya Mji Mdogo).

Hivyo mnaamriwa kuhudhuria wenyewe/mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
AMRI hiiimetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hii leo tarehe 11.03.2022

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MULEBA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MULEBA MKOA WA KAGERA**
**MAOMBI MADOGO NA. 15/2022**

ZEBADIA ZAKAYO……………………… MLETA MAOMBI
DHIDI YA
1.EDIPHONCE RUSENENE 2. ALISTIDES ANDREA
3.SIMON SIMON 4. VERIUS KILIMUGISHA
…………WAJIBU MAOMBI

KWA:1. ALISTIDES ANDREA 2. SIMON SIMON
3. VERIUS KILIMUGISHA

**(POPOTE PALE ULIPO)**

Mnaarifiwa kuwa Maombi Na.15/2022 yamepangwa kutajwa tarehe 22.04.2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza,J.K.Banturaki saa2.30 asubuhi,mahali-Muleba(Mamlaka ya Mji Mdogo).
Hivyo mnaamriwa kuhudhuria wenyewe/mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
AMRI hiiimetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hii leo tarehe 11.03.2022

………………………………………………
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MULEBA**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACKLINE GWALESHA KASONYI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne **index No S0241- 0054.** kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa kupitia KOWAK **GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/73159/2021.**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NEWTON MUJUNI MJUNGU**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye **NAMBA ZA USAJILI T.214 BSL.**
yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.
TAARIFA YA POLISI
**MBE/MBE/RB/148854/2022**

---

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY IN THE DISTRICT/MAGISTRATE COURT OF MULEBA**
**JUVENILE CIVIL APPLICATION CASE NO 3 OF 2022**
**CATHERINE CATHBERT …..APPELLANT/APPLICANT**
**BRASIO KAIZA PAULO……………………RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE OF MENTION/HEARING**

TAKE notice that the above case has been fixed for mention/hearing on 19 Day of April,2022 at 8.00 am Before Hon A.H.MWATINDWA SRM
YOUR ARE required to appear before this court witin fail and you must produce on that day all the documents upon you intend to rely in support of case.
Given under my hand and the Seal of The Court this 6 day of April 2022.

**RESIDENT MAGISTRATE**
**MULEBA**

---

**IN THE HIGH COURT OF**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA AT BUKOBA**
**MISC LAND CASE APPLICATION 91/2021**
**(Originating from Land No. 13 of 2019 of this Court, Original Land Application No. 46 of 2014 of the DLHT For Kagera at Bukoba)**
**BRAISON DAMIAN …………………APPLICANT**
**VERSUS**
**ANDASON DAMIAN & 3 OTHERS ……..RESPONDENT**
**TO; 1. ANDASON DAMIAN**
**2. MWEBEMBEZI DAMIAN**
**3. DAMIAN RAZARO**
**OF RUSHAKA VILLAGE KAAGYA WARD BUKOBA (R)**

**RE: NOTICE FOR DATE OF HEARING**

Whereas the above mentioned Applicant has lodged a case registered as Misc Land Application no. 91 of 2021 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.
Take notice that the above said case has been scheduled for hearing on 2nd day of May, 2022 at 08:30 am before Hon. Mwenda J. You are authorized to appear in person or through your Advocate.
Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said hearing the case will proceed in your absence.
Given under my hand and seal of the court this 13th day of April, 2022.

…………………………………
**A. W. KABUKA**
**DEPUTY REGISTRAR**
**HIGH COURT OF TANZANIA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NO.218 YA MWAKA 2010**
**ROBERT DAMIAN MUGISHAGWE…..MDAI**
**DHIDI YA**
**DAVID DICKSON MWAKAPANDA……..MDAIWA**
**KWA.DAVID DICKSON MWAKAPANDA**

**KUITWA SHAURINI**

Kwakuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya madai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii,kwahiyo mnahitajiwa kuhudhuria katika mahakama hii binafsi au kwa wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya arehe 20/4/2022 saa 7:00 mchana .kwa mujibu wa madai hayo na kwakuwa siku hiyo ni siku ya kukata shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

ANGALIA.
Kama hukuhudhuruia siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikithibitisha kama mmepokea kuitwa shaurini ,itaweza kutoa hukumu kuwa mmeshindwa.
**Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 31 mwezi wa MARCH/2022**

HAKIMU MKAZI
KISUTU -DAR ES SALAAM

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI BAJAJ BOXER

**FAIR DEAL AUTO PVT LTD**
anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki bajaj boxer yenye usajili namba **T350 CTV, CHASSIS NAMBA: MD2A21BZ3DWH78082, ENGINE NAMBA : PFZWDH42418.**
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/148530/2022**

---

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

MAKALA MAALUMU IJUMAA KUU

## PADRE JEROME NAPELLA:

# Hizi hapa salamu za Ijumaa Kuu, ina maana hii, tuisherehekee hivi

Na Christina Mwakangale

LEO ikiwa ni siku ya maombolezo kwa waumini wote wa Kikristo, Ijumaa Kuu ina tafsiri pana katika kuimarisha imani aliyopitia Bwana na Mwokozi Yesu, kuanzia mkesha wa maombi na wanafunzi wake kabla ya kukamatwa, kuteswa, kifo hadi kaburini.

Katika kuadhimisha siku hiyo, Nipashe imemtembelea Padre Jerome Napella wa Kanisa la Anglikana, Kristo Mfalme, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, ambaye anataja mambo saba yanayohusiana na siku hii, akiyaeleza yalivyo muhimu kwa tafsiri ya kiimani.

Anasema kanisa na Wakristo hukumbuka mengi, ingawa yapo ambayo hawayajui ipasavyo, ikiwamo tafsiri anazozitaja: Mateso, Usaliti, Kukanwa, Kutengwa na Wanafunzi Wake, Kuiabishwa na Kusulubiwa Msalabani Golgota.

Katika hatua hiyo, Padre Napella anaweka kituo cha mazungumzo, akianza na kutoa wito kwa Watanzania wote wenye mapenzi mema bila kujali tofauti za kiimani, kwamba ni wakati wa dunia kurejesha heshima yake kwa kuishi maisha ya kuheshimiana kwa kumhofia Mungu, akisisitiza kanuni 'jambo ambalo yeyote hatopenda kutendewa, asimtendee mwenzake."

Padre Jerome ambaye pia ni Padre anayeongoza Mtaa huo wa Kristo Mfalme, Kinondoni, anafafanua kuhusu siku hiyo, kwa kina kupitia mazungumzo yafuatayo na mwandishi wa makala hii:



Padre Napela. NA MPIGA PICHA WETU

**Mwandishi:** Nini tafsiri ya siku ya Ijumaa Kuu kiimani?

**Padre Jerome:** Siku hii ni ya huzuni na mwanzo wake unaanzia siku ya Jumatano ya Majivu na kufunga kwa siku 40, ambazo zinaelekea ukingoni na leo Yesu ndipo alipoingia kwenye mateso.

Siku ya Jumatano ya Majivu inapoanza, inawakumbusha Wakristo kupitia majivu, kwamba mwanadamu ni Mavumbi na Mavumbini atarejea. Ijumaa Kuu, Jumamosi hadi Jumapili anapofufuka ndipo huzuni inapoisha.

Kama Mkristo, unatakiwa uishi kwa namna gani katika siku 40 kwa kufunga, lakini si kwa siku hizo tu, inatakiwa uishi matendo mema siku zote.

Lakini, bado kuna changamoto kushughulika na wanadamu, ni jambo gumu kidogo! Wapo watu ambao ni 'so committed' (wana dhamira ya kweli) na wengine wanaona kawaida kipindi hiki, wapo wanaotii pia kipindi cha Kwaresma.

**Mwandishi:** Kufunga ina tafsiri gani kwa Mkristo, hasa kipindi cha Kwaresma?

**Padre Jerome:** Sisi kwetu, kufunga si kipindi cha Kwaresma tu, unaweza ukapanga mwenyewe nafunga wiki moja au siku tatu kwa ajili ya jambo fulani, Kwa hiyo, wanaona umuhimu wa Kwaresma kufunga na kuutia mwili adabu, lakini kujizoeza kufunga, pamoja na kwamba ni afya, kujisogeza karibu na uwapo wa Mungu.

Unapata nafasi ya kusali wewe binafsi na sio lazima watu wote wajue umefunga. Yesu alitupa maelekezo ya kufunga, akisema unapofunga usiwe kama watu wanafiki, kuongea na watu kwamba wewe umefunga. Jipake mafuta, kaa vizuri, wapo wanaopofunga hata baada ya Kwaresma, lakini hawataki wajulikane.

**Mwandishi:** Kila inapofika Ijumaa kuu, matukio kadhaa kupitia makanisa tofauti nchini huonyesha maigizo ya Yesu akiwa Msalabani, nini maana ya Msalaba?

**Padre Jerome:** Msalaba kwa kanisa ndiyo kilele cha imani siku ya Ijumaa Kuu, na kuleta ukombozi kwa mwanadamu. Akiwa Msalabani, Yesu alitamka maneno saba ambayo kila neno linabeba ujumbe wake. La kwanza baba uwasamehe kwa kuwa hawajui walitendalo...Ipo ibada ya kuuheshimu msalaba.

> “
>
> **Padre Jerome: Sisi kwetu, kufunga si kipindi cha Kwaresma tu, unaweza ukapanga mwenyewe nafunga wiki moja au siku tatu kwa ajili ya jambo fulani, Kwa hiyo, wanaona umuhimu wa Kwaresma kufunga na kuutia mwili adabu, lakini kujizoeza kufunga, pamoja na kwamba ni afya, kujisogeza karibu na uwapo wa Mungu.**

**Mwandishi:** Je, Kanisa lina utaratibu wa kuwajenga watoto ambacho ni kizazi kinachokua, kufahamu umuhimu wa hatua hii ya Kwaresma hadi Ijumaa Kuu?

**Padre Jerome:** Kwa kawadia kuna madarasa kwa ajili ya watoto Jumapili, kuhusu Kwaresma, mateso ya Kristo, wanafundishwa namna ya kuishi na wenyewe waendane na matendo mema.

**Mwandishi:** Una ujumbe gani kwa Wakristo wote nchini na umuhimu wa Kanisa?

**Padre Jerome:** Tunaishi katika dunia yenye changamoto sana.

Na moja kati ya kazi kubwa ya kanisa duniani ni kuirudishia dunia heshima yake iliyopotea, Mungu akaumba dunia na kila kitu unachotazama chema. Lakini, sasa huoni dunia hiyo ikifurahia huo uzuri wake, magonjwa, vita, mapigano, dhuluma na mauaji.

Kuna wakati huwa sitamani hata sitaki kuangalia vyombo vya habari, kwa sababu hakuna habari njema siku nyingine, huku watu wamekufa, Mzee wa miaka 54 abaka mjukuu. Niwaombe watu wote kuyaishi maisha ya kama Mungu anavyotaka. Maisha ni zawadi kutoka kwa Mungu, Kila mtu aone thamani ya kuwa mwanadamu. Tuwaheshimu wengine na tudumishe amani.

**Mwandishi:** Je, una jambo lolote la kueleza ambalo ulitamani kulisema kupitia vyombo vya habari na bado hujafanya hivyo?

**Padre Jerome:** Nina mambo mengi ya kusema, lakini niseme jambo moja. Watanzania wafurahi kuwa Watanzania, watunze tunu za nchi yetu, tuheshimiane bila kujali tofauti zetu za dini, rangi, vyama. Inakuja 'issue' (suala) ya kuwa Mtanzania, tuwe Watanzania.

Nakumbuka nikiwa mdogo, baba yangu alikuwa mwalimu. Watu wa zamani watakumbuka kulikuwa na picha ya mwalimu, akiwa amenyoosha kidole. Siyasahau maneno yaliyokuwa yameandikwa pale yakisema 'timiza wajibu wako, wakati ni huu,' Watu wayaenzi yale maisha ambayo tumeyaishi kwa miaka yote.

# LUSAJO HAJAMKATIA TAMAA MAYELE

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA na kinara wa ufungaji mabao kwenye klabu ya Namungo FC, Reliants Lusajo amesema kuwa bado anapambana na hajakata tamaa kukifukuzia kiatu cha ufungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ingawa amekiri kuna ugumu kutokana na mastraika wengi kufanya vizuri.

Lusajo ambaye hadi sasa ametikisa nyavu mara 10, bao moja nyuma ya kinara Fiston Mayele wa Yanga, amesema msimu huu mbio za ufungaji bora zimekuwa ngumu, hivyo zinahitajika jitihada kubwa ili mchezaji yoyote kuibuka kinara msimu huu.

"Ushindani ni mkubwa sana, kuna watu walikuwa chini huko, kwa sasa wanafunga na kutukaribia, hata aliye juu hajawazidi wa chini yake mabao mengi, kwa hiyo kuna mchuano mkali. Kwangu mimi naona mbio za kiatu cha dhahabu ni ngumu msimu huu na imechangiwa zaidi kutokana na ligi yenyewe kuwa ngumu," alisema Lusajo.

Alisema kuwa yeye mwenyewe ataendelea kupambana, akifanya jitihada kwa kushirikiana na wachezaji wenzake ili kutimiza ndoto aliyojiwekea.

"Ndoto yangu ni kuwa mfungaji bora siku moja, kwa hiyo kama msimu huu nikiupata nitakuwa nimetimiza ndoto yangu na kuisaidia pia timu yangu ya Namungo," alisema.

Lusajo ambaye kuna wakati alikuwa kinara wa ufungaji amepitwa bao moja na Mayele ambaye kwa sasa ni kinara akiwa na mabao 11, huku George Mpole wa Geita Gold akishika nafasi ya tatu kwa kuwa na mabao tisa.




Wachezaji wakichuana kwenye mashindano ya Ligi ya Mchangani, maarufu Betika Sodo Bingwa Ligi yanayoendelea kwenye mikoa sita nchini. **PICHA: SAADA AKIDA**

# *Ligi ya Betika Sodo yachanja mbuga*

**Na Saada Akida**

MATOKEO ya sare yametawala kwenye mechi za kwanza za raundi ya pili ya Ligi ya Mchangani 'Betika Sodo Bingwa Ligi' inayochezwa kwenye mikoa sita nchini.

Kwenye mechi za ufunguzi wa raundi ya pili, katika kituo cha Dar es Salaam, matokeo ya sare kutawala huku, Espanyola ikipata ushindi na pointi tatu zilizowaimarisha kileleni mwa msimamo na kufikisha pointi 20, ikifuatiwa na Care Boys ambayo ililazimishwa sare ya mabao 3-3 na Smart Fighter.

Katika mchezo huo, shujaa wa timu ya Smart Fighter alikuwa Mohammed Salum aliyefunga mabao mawili ya kusawazisha kwa timu yake huku Said Ahmed akifunga moja.

Kwa upande wa timu ya Care Boys yalifungwa na Husein Taidini, Hassan Songoro na Kassim Mohammed huku timu hiyo ikivuna pointi moja na kupanda hadi nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi hiyo inayodhaminiwa na Kampuni ya Michezo ya kubashiri ya Betika.

Wakati Morocco Square inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo ikiwa na pointi 14 kwenye mchezo uliopita ilitoa kipigo cha mabao 3-0 kwa Swazi Inter. Hadi sasa timu zote zimecheza mechi nane, saba za mzunguko wa kwanza na moja ya mzunguko wa pili, huku Hard Number ikigawana pointi moja moja na Jaga FC baada ya sare ya bao 1-1 katika mchezo uliopita.

Meneja masoko wa Betika, Nelson Mwanuzi alisema hamasa imekuwa kubwa kwa vijana kuchuana na kuonesha vipaji vyao vya soka kwenye Ligi hiyo inayochezwa kwenye mikoa sita nchini.

"Mbali na Dar es Salaam, mikoa mingine ni Mwanza, Ruvuma, Iringa na Kilimanjaro na Lindi," alisema.

Alisema mikoa yote hiyo Sodo inachezwa kwa kiwango ubora na upinzani wa hali ya juu, lengo kubwa ni kuibua vipaji, pia kufanya kazi kwa karibu na wateja wetu wa Betika kote nchini.

## Mbeya City yapania nne bora

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule amesema moja ya mipango yake ni kuona timu yake inafanya vizuri na kuwa miongoni mwa timu nne ambazo zitapata nafasi ya kwenda kucheza michuano ya Kimataifa, ikiwemo Kombe la Shirikisho Afrika, (CAF) kwa msimu ujao.

Tanzania imefanikiwa kupata pointi ambazo zitapeleka timu nne kwenye michuano ya Kimataifa mbili zitacheza Shirikisho na nyingine kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika, baada ya Simba kufanikiwa kutinga hatua ya robo ya michuano ya CAF mwaka huu.

Mbeya City inashika nafasi ya tano ikiwa na poiti 25 wakiwa chini ya Namungo FC ambao wako nafasi ya nne wakikusanya pointi 26 na Azam FC wanashikilia nafasi ya tatu kwa kukusanya alama 28 na timu zote zikiwa zimecheza michezo 19 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Lule alisema ana matarajio makubwa na wachezaji wake kujituma na kuwa makini katika kufuata kile anachowapa katika mazoezi na kuhamishia uwanjani kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yao.

Alisema malengo yake ya awali ni kuhakikisha timu hiyo inaendelea kuwepo katika ligi na kufanikiwa jambo hilo sasa anahitaji kupambana kuhakikisha anamaliza katika nafasi tatu au nne za juu.

"Nitashindwa kushika nafasi mbili za juu, lakini kuanzia tatu na nne nina imani nitaweza kuzishika," alisema Lule.

Alikiri kuwepo na mapungufu katika kikosi chake na kufanyia kazi kila sehemu ili kufanikiwa malengo yao ya kushinda mechi zote zilizobakia za mzunguko wa pili ili kufikia malengo yao ya kumaliza katika nafasi tatu au nne za juu.

## Pamela aamua kuangusha moja moja

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya kimya cha muda mrefu, mwimbaji wa nyimbo za Injili Pamela Tumaini, amefyatua wimbo alioupa jina la 'Suprise' ikiwa ni mwendelezo wa kurekodi nyimbo za albamu yake ya pili alioipa jina la 'Pigana Nao'.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, mwimbaji huyo amesema, tangu aandae albamu ya kwanza ya Kipimo cha Imani mwaka 2016 alikuwa kimya na sasa ameibuka upya.

"Nimekuja na mtindo wa kurekodi wimbo mmoja baada ya mwingine hadi nikamilishe albamu ya pili kwani zipo nyingi, lakini nimeamua kuanza na huu wa 'Suprise'," amesema Pamela.

Akifafanua zaidi, amesema ujumbe wa wimbo huo unakumbusha watu kuwa Mungu siku zote huwa anawawazia amema, na pale ambapo akili zao zinapofikia ukomo kuwaza ndipo Mungu huanzia.

"Nilikuwa kimya kwa muda mrefu na sasa mwaka huu nimeibuka upya baada ya kusoma soko la muziki wa Injili na sasa nimeona ni wakati mwafaka wa kurudi upya kumwimbia Mungu," amesema.

Mwimbaji huyo ametaja baadhi ya nyimbo za albamu yake ya kwanza alizotamba nazo kuwa ni 'Hakuna Kama Wewe, Kifo Hakina Huruma, Amenitoa Mbali na Mfanyie Mungu Kazi'.

"Kwa upande wa nyimbo za albamu ya pili, mbali na Suprise na Pigana Nao, zipo nyingine kama 'Saa ya Bwana na Bwana ndiye Mchungaji Wangu' ambazo nitaendelea kurekodi mmoja baada ya mwingine," amesema.

Pamela amesema amesoma soko la muziki wa Injili kwa kipindi chote ambacho alikuwa kimya, na sasa anaamini kuwa hatasimama tena badala yake atafyatua nyingi kadri inavyowezekana.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SALAH MSHAHARA MKUBWA

LIVERPOOL imekubali kumlipa mshambuliaji Mohamed Salah pauni 400,000 kwa wiki ili kumshawishi nahodha huyo wa Misri kubaki Anfield. (***Metro, via Football Insider***)

### FERNANDINHO AGOMBEWA

KLABU za Corinthians, Botafogo na Flamengo zimewasiliana na nahodha wa Manchester City, Fernandinho kuhusu uhamisho wa msimu ujao baada ya tangazo la kushitukiza la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 la kuondoka Etihad. Lakini kiungo huyo wa kati Mbrazili anapendela kurejea katika klabu yake ya zamani ya Athletico Paranaense. (***Globo Esporte***)

### HAG SAFI MAN

KLABU ya Manchester United imefikia "makubaliano kwa maneno" na kocha wa Ajax Erik ten Hag kuwa kocha wao ajaye. Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 52, anatarajiwa kujiunga nao kwa mkataba wa miaka minne, lakini tangazo halitatolewa kabla Ajax kukabiliana na PSV Eindhoven katika mchezo wa fainali ya kombe la Uholanzi Jumapili. (***Athletic***)

### NKUNKU KWENYE RADA

MANCHESTER United pia wanaangalia uwezekano wa kumhamisha kiungo wa kati wa RB Leipzig na Ufaransa, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24, ambaye amefunga mabao 17 na kusaidia 12 katika mechi 29 za msimu huu za ligi ya Ujerumani, Bundesliga . (***Florian Plettenberg***)

### JOHNSTONE AGOMBEWA

KLABU za Manchester United na Tottenham Hotspur kwa pamoja zinamuwania mlinda lango wa West Brom na England mwenye umri wa miaka 29, Sam Johnstone msimu huu. (***Sky Sports***)

### GABRIEL ATAKIWA BARCA

KLABU ya Barcelona wanamlenga nyota wa Arsenal na Brazil, Gabriel mwenye umri wa miaka 24. (***Sport***)

### BREMER AWINDWA LIVERPOOL

LIVERPOOL wako tayari kutoa ofa ya pauni milioni 25 kwa ajili ya mlinzi Mbrazili kutoka klabu ya Torino, Gleison Bremer ambapo Januari tayari walikuwa wameelezea nia yao kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. (***Tuttomercato***)

### DE LIGT AWANIWA BARCA

BARCELONA lazima iilipe Juventus euro milioni 100 kama wanataka kumsajili mlizni wa kati wa Uholanzi, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 22. (***Fichajes***)

### OSIMHEN KUBAKIZWA

NAPOLI wameazimia kuendelea kumshikilia mfungaji wao wa mabao, Victor Osimhen msimu huu licha ya mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 23 kusakwa na klabu za Manchester United na Arsenal. (***Teamtalk***)

### GINTER AWANIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa imeonesha nia yake ya kumtaka mchezaji wa Ujerumani, Matthias Ginter, ambaye mkataba wake kule Borussia Monchengladbach unamalizika mwishoni mwa msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 amekuwa akisakwa na Juventus, Tottenham na West Ham. (***Sky Sports***)

### ERIKSEN AGOMBEWA

KLABU ya Brentford ina matumaini mchezaji wa Denmark, Christian Eriksen ataendelea kubaikia katika klabu hiyo baada ya kumalizika kwa mkataba wake wa miezi sita, lakini wanakabiliwa na "ushindani mkali" katika kupata saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miakaa 30 kutoka timu yake ya zamani ya Tottenham. (***90Min***).

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# PEP: MAN CITY IPO KWENYE MATATIZO

**Ni baada ya kufuzu nusu fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya, yakumbwa na majeruhi kibao...**

**MADRID,** HISPANIA

PEP Guardiola amesema majeraha waliyopata Manchester City wakati wakifuzu nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atletico Madrid yameiacha timu yake kwenye "shida kubwa."

Sare ya bila kufungana katika mji mkuu wa Hispania, Madrid, ilifanikisha ushindi wa jumla wa 1-0 na kupelekea City kufuzu nusu fainali ya tatu katika historia ya klabu hiyo na sasa watakutana na washindi mara 13, Real Madrid.

Lakini huku mechi ya Jumamosi ya nusu-fainali ya Kombe la FA dhidi ya Liverpool ikikaribia, maendeleo ya City yaliwagharimu, Kevin de Bruyne na Kyle Walker walioondoka uwanjani wakiwa mejeruhi, na Phil Foden akihitaji kufungwa bandeji kichwani pale kwenye Uwanja wa Wanda Metropolitano.

"Tuko kwenye matatizo makubwa," alisema Guardiola akiiambia BT Sport.

"Hatuwezi kusahau tulicheza siku tatu zilizopita mchezo mgumu dhidi ya Liverpool. Tulikuja hapa, tuna majeruhi wengi.

> **"Sijui nini kitatokea wiki zi jazo, lakini leo (juzi) tu naenda kusherehekea, ni mara ya tatu katika historia ya Manchester City kufika nusu fainali ya Ligi ya Ma bingwa Ulaya, na ni mafani kio makubwa kwetu."**

Guardiola hakutaja jinsi majeraha yalivyokuwa makali, huku akidai pia "Hakuwa na la kusema" kwenye matukio hayo mabaya ambayo yaliharibu maendeleo ya kikosi chake Jumatano usiku.

Mechi hiyo iliisha kwa mbwembwe na uchungu na mikwaruzano uwanjani.

Kwanza vurumai iliyohusisha wachezaji wengi kutoka pande zote mbili ilizuka uwanjani baada ya Felipe kumpiga teke Foden.

Miongoni mwa matatizo mlinzi wa Atletico, Stefan Savic alimvuta nywele mchezaji wa akiba wa City, Jack Grealish baada ya wawili hao kurushiana maneno, huku Felipe akitolewa nje.

Matatizo hayo yaliendelea baada ya timu hizo kuondoka uwanjani huku wachezaji wakihitaji kutengwa. Picha za televisheni zilionyesha vitu vikirushwa na polisi waliripotiwa kuhusika kurejesha utulivu.

Alipoulizwa kuhusu matukio hayo katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi, Guardiola alisema tu "hana la kusema".

Akiwa amebanwa zaidi kuhusiana na jeraha la kichwa alilopata Foden katika changamoto nyingine mbaya kutoka kwa Felipe katika kipindi cha kwanza, Guardiola alisema: "Sizungumzi kuhusu waamuzi au wapinzani pia."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,144

MECHI KALI
SHEFFIELD UTD
VERSUS
READING
1 | 1.56
X | 3.97
2 | 5.36

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ILIBAKI KIDOGO XHAKA ATIMKE ARSENAL

**LONDON, England**

GRANIT Xhaka amesema wachezaji na mashabiki wanahitaji kutendeana kwa "uaminifu na heshima" zaidi baada ya kukiri kwamba alikuwa karibu kuiacha Arsenal kwa sababu ya "chuki kubwa" aliyokuwa akiipata.

Xhaka alisema "mabegi yake yalishafungwa" muda mfupi baada ya makabiliano ya hasira na mashabiki wake Oktoba mwaka 2019.

"Ninapofumba macho sasa, bado ninaweza kuona sura zao. Ninaweza kuona hasira zao," alisema Xhaka akiiambia BBC Sport.

"Hati za kusafiria zilikuwa tayari. Nilikuwa nimemalizana na Arsenal. Nimemaliza."

Tukio hilo lilitokea wakati Xhaka alipokejeliwa na mashabiki wake alipotolewa wakati wa mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Crystal Palace kwenye Uwanja wa Emirates.

Xhaka aliitikia kwa kupunga mkono na kutega sikio lake kwa dhihaka, na mashabiki walitupa jezi zake chini.

"Nilikuwa nimeanza kusogea niliposikia kelele. Na hawakuwa watu wachache tu kwenye kona - kulikuwa na watu wengi. Nilishtuka. Sijawahi kupata kitu kama hiki," alisema Xhaka. "Hii ni chuki."

Moja ya shutuma zinazoelekezwa kwa Xhaka mara kwa mara na mashabiki wa Arsenal ni utovu wake wa nidhamu, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 akiwa amelimwa kadi nyekundu mara tano tangu ajiunge na Washikabunduki hao kutoka Borussia Monchengladbach mwaka 2016.

# Werner: Nilidhani Chelsea tumefuzu

**MADRID, Hispania**

TIMO Werner aliyehuzunishwa alidhani Chelsea walikuwa wamekamilisha kazi yao kwa njia isiyowezekana alipofunga bao la tatu kwenye Uwanja wa Bernabeu, Jumanne usiku.

Wakiwa wameteleza kwa kichapo cha mabao 3-1 wiki iliyopita, The Blues walipambana nyumbani kwa Real Madrid huku wakionekana kufanya jambo lisilofikirika ili kujikatia tiketi ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Huku Mason Mount ikianza kufunga bao la kwanza dakika ya 15, mpira wa kichwa wa Antonio Rudiger uliwafanya vijana hao wa Thomas Tuchel kuwa mbele kwa mabao mawili.

Juhudi nzuri za Werner pekee ziliwafanya wageni kutawala kwa dakika 15 za kucheza akifunga la tatu, lakini bao la Rodrygo aliyetokea benchi katika dakika ya 80 lilipelekea sare ya dakika za nyongeza, wakati mpira wa kichwa wa Karim Benzema ulipothibitika kuwa wa maana.

Akitafakari juu ya kushindwa kwa jumla ya 5-4, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani alisema: "Niliposherehekea (lengo langu] nilifikiri ndivyo hivyo.

"Tungeweza kufunga kabla ya hapo na kufanya matokeo kuwa 3-0 lakini mambo yalikuwa tofauti.

"Ni jambo ambalo unaweza kulizungumzia, lakini nilipofunga nilifikiri tumemaliza kazi.

"Tulikaribia kutoipa Madrid nafasi, lakini mwishowe lazima tuseme mabao waliyofunga yalikuwa mazuri sana."

"Tulikuwa na kila kitu tulichohitaji 3-0, tulikuwa na nafasi ya kupitia.

"Lakini mwishowe huwezi kuwazuia Madrid kwa muda wote. Lakini tulijaribu kila kitu katika muda wa kawaida na muda wa ziada.

"Hii (mechi ya ugenini) ilikuwa nzuri kwetu, kwa hivyo tumesikitishwa sana baada ya kile tulichoweka kwenye mchezo huu na jinsi tulivyocheza.

"Tulikuwa na mchezo mzuri na tulikuwa na dakika 10 za kumaliza ili



## HABARI MICHEZO

4,195,580

# SIMBA INAWEZA KUITOA ORLANDO

**Dennis Fussi**

KOCHA wa zamani wa makipa wa klabu ya Simba, Mwarami Mohamed amesema anaamini timu hiyo itaibuka na ushindi Jumapili katika mchezo wa Robo Fainali wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini.

Kocha huyo amesema kinachompa matumaini ni rekodi ambayo imejiwekea timu hiyo inapocheza nyumbani kwenye michuano hiyo na maandalizi ambayo inayafanya.

"Katika suala na michuano ya kimataifa kwenye Uwanja wa Mkapa kwa Simba sina hofu hata kidogo, nina uhakika Simba itashinda sijui idadi ya mabao, lakini ushindi upo," amesema Mwarami.

Kocha huyo ambaye pia aliwahi kuitumikia timu ya Taifa 'Taifa Stars', amesema kwa uzoefu wake akiwa na timu hiyo, haoni wapinzani wao Pirates kama wataweza kupata hata bao moja kutokana na mikakati iliyopo.

Amesema Simba ni tofauti na klabu nyingi za Tanzania, hasa katika mashindano ya kimataifa, hivyo amewaomba mashabiki kuondoa hofu na kujitokeza kwa wingi Jumapili kwenda kuishangilia timu yao.



Wafanyakazi wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) wakishiriki katikambio za Run 4 Autusim zenye lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya watoto wenye Usonji zilizoandaliwa na Lukiza Foundation zilizofanyika hivi karibuni Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kuna vita kumsajili Adebayor-Simba

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba ikiwa mbioni kutaka kumsajili winga matata wa US Gendermarie ya Niger, Victorien Adebayor, tayari klabu kadhaa zikiongozwa na RS Berkane zimeingia vitani kuiwania saini ya mchezaji huyo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu ya Simba, Ahmed Ally amesema jana kuwa wameanza kutunishiana misuli na baadhi ya klabu ambazo nazo zimeanza kumshawishi mchezaji huyo kwa dau nono, hivyo kwa sasa hawapo peke yao sokoni kumhitaji mchezaji huyo.

"Tunamtaka sana Adebayor, ni mchezaji mzuri, na mchezaji yoyote akiwa mzuri ni lazima kuwe na vita sokoni, tunajaribu kutunishiana misuli na klabu mbalimbali, lakini waswahili wanasema kila mtu anajikuna anapoweza," alisema Meneja huyo.

Alisema mchezaji huyo tayari ameingia kwenye midomo na mashabiki na mawakala wengi Afrika, hivyo thamani yake imepanda ghafla sokoni, tofauti na awali.

"Unajua ameshaingia midomoni mwa mawakala, thamani yake imepanda sana na wanazidi kuipandisha sokoni, na hii ni kwa sababu amejitangaza sana kwa uwezo wake, lakini sisi Simba tunaendelea kupambana, kutunishiana misuli na klabu kubwa, unajua ukiwa unamsajili mchezaji sokoni halafu upo peke yako, hakuna hata anayemhitaji ujue unakwenda 'kupigwa'. Kwa hiyo tunaendelea kupambana, tukimkosa sawa, na tukimpata tutashangilia," alisema Ahmed.

Moja ya klabu inayotajwa kuwa mstari wa mbele kutaka kumsajili mchezaji huyo niu RS Berkane ya Morocco ambayo inadaiwa kumuahidi wakala wake pesa nyingi kama akifanikisha jambo hilo.

Hata hivyo, Adebayor mwenyewe amekuwa akionyesha mapenzi dhahiri kwa klabu ya Simba, akiposti picha mbalimbali alizopiga nchini, ikiwa ni ile video fupi ya mashabiki wa Simba wakimshangilia na kumuimba, mwenyewe akionekana kufurahia na hata maelezo yake mafupi kwenye mtandao wake wa kijamii, alionyesha kushangazwa na kufurahia mapokezi na heshima kubwa aliyoipata kutoka kwa mashabiki wa klabu hiyo.

Mchezaji huyo alionyesha kiwango cha hali ya juu kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, hatua ya makundi akiwa na klabu hiyo ya Niger, akipachika mabao sita na kuwa mmoja wa wachezaji wanaowania kiatu cha dhahabu kwenye michuano hiyo.


# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 16/04/2022 | 17:00 | Watford vs Brentford | 2.66 | 3.16 | 2.66 |
| 02. 16/04/2022 | 17:15 | Alaves vs Rayo Vallecano | 2.57 | 3.03 | 2.93 |
| 03. 16/04/2022 | 17:30 | Manchester City vs Liverpool | 2.35 | 3.21 | 2.96 |
| 04. 16/04/2022 | 18:00 | St Etienne vs Brest | 2.31 | 3.21 | 3.11 |
| 05. 16/04/2022 | 20:00 | Dijon vs AC Ajaccio | 2.31 | 3.10 | 3.15 |
| 06. 16/04/2022 | 20:00 | Nimes vs Sochaux | 2.44 | 3.15 | 2.90 |
| 07. 16/04/2022 | 20:00 | Valenciennes vs Le Havre | 2.65 | 3.15 | 2.65 |
| 08. 17/04/2022 | 16:00 | Metz vs Clermont Foot | 2.65 | 3.15 | 2.70 |
| 09. 17/04/2022 | 16:15 | Newcastle vs Leicester | 2.50 | 3.20 | 2.80 |
| 10. 17/04/2022 | 18:30 | Union Berlin vs Eintracht Frankfurt | 2.38 | 3.26 | 2.91 |
| 11. 17/04/2022 | 20:30 | Bayer Leverkusen vs RB Leipzig | 2.71 | 3.41 | 2.46 |
| 12. 17/04/2022 | 20:30 | Giresunspor vs Besiktas | 2.88 | 3.28 | 2.36 |
| 13. 17/04/2022 | 22:00 | Sevilla FC vs Real Madrid | 3.19 | 3.19 | 2.31 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 15/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 4465 | Luton Town vs Nottingham | 2.77 | 3.17 | 2.48 |
| 16:00 | 2522 | Hammarby vs Mjallby | 1.48 | 4.10 | 5.47 |
| 16:00 | 5591 | Gabala vs FK Sumgayit | 1.69 | 3.50 | 4.47 |
| 17:00 | 1049 | Pyunik Yerevan vs Alashkert Martuni | 1.77 | 3.26 | 4.38 |
| 17:00 | 2047 | Hull City vs Cardiff | 2.47 | 3.12 | 2.82 |
| 17:00 | 2503 | Swansea vs Barnsley | 1.70 | 3.56 | 4.74 |
| 17:00 | 3767 | Bournemouth vs Middlesbrough | 1.99 | 3.28 | 3.68 |
| 17:00 | 3903 | Birmingham vs Coventry | 2.97 | 3.27 | 2.29 |
| 17:00 | 4639 | Sheffield Utd vs Reading | 1.56 | 3.97 | 5.36 |
| 17:00 | 4889 | Stoke City vs Bristol City | 1.75 | 3.58 | 4.37 |
| 17:00 | 5273 | Preston vs Millwall | 2.36 | 3.02 | 3.07 |
| 17:00 | 5426 | Peterborough vs Blackburn | 4.44 | 3.50 | 1.76 |
| 17:00 | 5493 | West Bromwich vs Blackpool | 1.71 | 3.52 | 4.76 |
| 17:30 | 2910 | FC Arouca vs Santa Clara | 2.42 | 3.07 | 2.97 |
| 18:00 | 4784 | KuPS Kuopio vs Seinajoen JK | 1.70 | 3.51 | 4.38 |
| 18:30 | 4218 | Karabakh vs Keshla FK | 1.14 | 6.22 | 16.53 |
| 18:45 | 1698 | Santiago Morning vs Arturo Fernandez Vial | 2.13 | 2.97 | 3.41 |
| 19:00 | 4345 | Dinamo Zagreb vs Istra | 1.21 | 5.61 | 10.63 |
| 19:00 | 5219 | Nordsjalland vs Sonderjyske | 1.82 | 3.54 | 4.09 |
| 19:30 | 4608 | Eibar vs Las Palmas UD | 2.08 | 3.26 | 3.41 |
| 19:30 | 4933 | Huddersfield vs QPR | 1.98 | 3.36 | 3.61 |
| 19:30 | 5068 | Dinamo Moscow vs Akhmat Grozny | 1.80 | 3.51 | 4.16 |
| 20:00 | 1881 | Famalicao vs Gil Vicente | 2.32 | 3.18 | 3.03 |
| 20:00 | 4690 | Spezia vs Inter | 8.78 | 5.39 | 1.30 |
| 20:30 | 4323 | Kayserispor vs Caykur Rizespor | 2.03 | 3.43 | 3.43 |
| 20:30 | 5733 | Trabzonspor vs Fatih Karagumruk | 1.48 | 4.28 | 5.97 |
| 21:00 | 4746 | Debreceni VSC vs Gyirmot FC | 2.00 | 3.31 | 3.35 |
| 21:00 | 4752 | CSD Barnechea vs Rangers | 2.96 | 3.06 | 2.30 |
| 21:05 | 3791 | Hajduk Split vs HNK Gorica | 1.34 | 4.68 | 7.22 |
| 21:15 | 5053 | Maribor vs NK Radomlje | 1.49 | 4.07 | 5.43 |
| 21:45 | 1576 | Bohemians FC vs Finn Harps | 1.70 | 3.51 | 4.38 |
| 21:45 | 2279 | Derry City vs Shelbourne | 1.48 | 3.71 | 6.44 |
| 21:45 | 2506 | UCD Dublin vs Drogheda Utd | 2.72 | 3.11 | 2.43 |
| 21:45 | 3282 | Inverness vs Kilmarnock | 2.86 | 3.05 | 2.45 |
| 21:45 | 3389 | Dundalk FC vs Sligo Rovers | 2.09 | 3.17 | 3.26 |
| 21:45 | 4100 | Linfield Belfast vs Glentoran Belfast | 2.00 | 3.26 | 3.41 |
| 21:45 | 5515 | Waterford Utd vs Galway United | 1.92 | 3.36 | 3.56 |
| 22:00 | 1619 | AC Milan vs Genoa | 1.32 | 4.90 | 9.20 |
| 22:00 | 1683 | Derby vs Fulham | 5.74 | 3.71 | 1.57 |
| 22:00 | 2315 | Real Sociedad vs Betis | 2.13 | 3.38 | 3.38 |
| 22:00 | 2746 | Rennes vs Monaco | 2.09 | 3.46 | 3.36 |
| 22:00 | 3501 | Danubio FC vs CA Boston River | 2.19 | 3.20 | 3.01 |
| 22:00 | 4268 | Shamrock Rovers vs St Patricks | 1.55 | 3.68 | 5.43 |
| 22:00 | 4689 | Amorebieta vs Mirandes | 2.37 | 3.11 | 2.97 |
| 22:30 | 1181 | Ceramica Cleopatra vs Coca Cola | 3.17 | 2.82 | 2.47 |
| 22:30 | 3244 | CA Tigre vs Huracan | 1.86 | 3.21 | 3.99 |
| 22:30 | 3384 | Vitoria Guimaraes vs Pacos Ferreira | 1.77 | 3.55 | 4.40 |
| 22:30 | 4770 | Ghazl EL Mahallah vs El Gouna | 2.39 | 2.80 | 3.35 |
| 23:30 | 2606 | UTC Cajamarca vs Academia Cantolao | 1.67 | 3.56 | 4.58 |
| 23:30 | 3187 | La Serena vs Union Espanola | 3.12 | 3.36 | 2.08 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Aprili 15, 2022

Nipashe




## Pep: Man City ipo kwenye matatizo



Wachezaji wa Manchester City wakishangilia baada ya kutoka suluhu na Atletico Madrid na kufuzu hatua ya nusu fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya, juzi. **PICHA: MTANDAO**

# MAUNDA ZORRO KUZIKWA KESHO

## ●●●Ajali ya gari yasitisha uhai wake wakati akitoka kwenye msiba ...

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI wa Bongofleva, Maunda Zorro aliyefariki kwa ajali ya gari Kigamboni, usiku wa kuamkia jana, anatarajiwa kuzikwa kesho katika makaburi ya Kongowe ya Mbagala mkoani Dar es Salaam.

Kaka wa marehemu, Banana Zorro aliliambia gazeti hili kuwa, msiba upo nyumbani kwa baba yao mzazi, Zahir Ally Zorro eneo la Maweni Kigamboni, na kwamba marehemu ameacha watoto watatu.

"Maziko ya mdogo wangu Maunda yatafanyika siku ya Jumamosi, katika makaburi ya Kongowe, kwa sasa shughuli zote za msiba zipo nyumbani kwa baba yetu mzee Zorro eneo la Maweni Kigamboni," alisema Banana.



Maunda amewahi kutamba na nyimbo mbalimbali za muziki wa kizazi kipya zikiwamo za 'Nataka Niwe Wako', Mapenzi ya Wawili' na nyingine nyingi zilizompa umaarufu katika muziki huo.

Hata hivyo, baadaye alikaa kimya kwa muda mrefu bila kutoa nyimbo mpya hadi umauti ulipomkuta baada ya kupata ajali wakati akitokea kwenye msiba wa rafiki wa muda mrefu wa familia yao.

Kwamba gari alilokuwa akiendesha msanii huyo liligongana na lori la mchanga na kusababisha kifo cha msanii huyo aliyejizolea sifa kwenye muziki kama ilivyo kaka yake Banana ambao wote wamerithi kipaji cha baba yao.

Baba wa marehemu mzee Zahir Ally Zorro, ni miongoni mwa wanamnuziki wakongwe nchini ambaye amewahi kutikisa kwa nyimbo mbalimbali zikiwamo za Cleopatra, Haifai Kabwe, Arua na Tikisa'.

Zorro amewahi kutumikia bendi mbalimbali ikiwamo ya Mass Media iliokuwa ikitumia mtindo wa 'Changa Wangu Baisikeli', ambayo ilipata umaarufu miaka ya 90 kwa muda mfupi ikasambaratika.

# Simba haiwazii mechi ya Yanga

**Na Saada Akida**

MENEJA wa Idara ya Habari na mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally amesema sasa akili na nguvu zao wanazielekeza katika mchezo wa robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Orlando Pirates.

Amesema hawaifikirii kabisa mechi yao ya Ligi dhidi ya Watani wao wa jadi Yanga itakayopigwa Aprili 30 mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana Ahmed alisema kwa sasa Simba inawaza michezo mikubwa miwili dhidi ya Orlando Pirates utakaopigwa Jumapili hii na baadae kurudiana nchini Afrika Kusini.

Alisema Yanga lazima watakaa na kuwaza mechi dhidi yao kwa sababu hawana mechi kubwa zaidi ya pambano hilo la watani wa jadi (Kariakoo Derby), wakati Simba wana mechi kubwa za kimataifa.

"Yanga wao wanatuwaza sisi, Simba haina muda wa kuwaza Kariakoo Derby kwa sababu ina mechi kubwa mbili dhidi ya Orlando Pirates nyumbani na ugenini baada ya hapo ndio tutaanza kufikiria mechi hiyo," alisema Ahmed.

Alisema Yanga lazima watumie muda mwingi kwa sasa kuiwaza mechi hiyo hali ya kuwa timu hiyo haina mechi kubwa zaidi ya kucheza zaidi ya kikosi cha wekundu wa Msimbazi hao ambao wao kwa sasa wanafikiria kumfunga Orlando Pirates ili kutinga nusu fainali.

"Baada ya kutinga nusu fainali ya Afrika ndio tutakuja kuwaza ligi yetu ya kubishana bishana ila kwa sasa nguvu zetu ziko katika michezo hiyo miwili," alisema Ahmed Ally na aliongeza

"Mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani kwa sababu jumapili hii tuna jukumu kubwa kuhakikisha Orlando Pirates hawachomoki Benjamin Mkapa, tunahitaji ushindi twende uwanjani tukasapoti Simba yetu kuhakikisha msimu huu tunaenda kucheza nusu fainali," alisema Ahmed.

Wakati huo huo Kiungo mshambuliaji wa Simba, Hassan Dilunga ameondoka nchini kueleke Afrika Kusini kwa ajili ya matibabu ya majeraha yanayomsumbua.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kitengo cha habari cha klabu hiyo, kilisema kutokana na vipimo alivyofanyiwa na madaktari, Dilunga anatakiwa kufanyiwa upasuaji na atakuwa Afrika Kusini kwa muda wa wiki tatu au nne.

Dilunga amekuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu anaenda nchini humo kwa ajili ya matibabu na huenda asionekana uwanjani kwa kipindi kilichobaki msimu huu.

Nyota huyo alisema ameushukuru uongozi wa klabu wa kugharamia matibabu hayo ambapo anaamini atarejea akiwa fiti kuitumikia timu.

"Kwanza nashukuru uongozi wangu kunipeleka Afrika Kusini kwa ajili ya matibabu ni jambo jema, naamini nitarudi nikiwa fiti kuitumikia timu yangu," alisema Dilunga.

Nyota huyo ameitakia heri timu yake kuelekea mchezo wa robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Orlando Pirates.

"Naitakia heri timu katika mchezo wetu muhimu wa nyumbani dhidi ya Orlando, nawaomba wachezaji wenzangu wapambane najua watanzania wako nyuma yao,"alisema Dilunga.

Dilunga amewaomba mashabiki kujitokeza kwa wingi na kuujuza uwanja siku ya Jumapili ili kuhamasisha wachezaji.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >